UBORA WA MAUDHUI YA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA 2022

Hali ya Uripoti wa Habari Tanzania

2022

https://sjmc.udsm.ac.tz/yearbook

WATAFITI
Abdallah Katunzi
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma

Christoph Spurk
Spurk Media Consulting Ltd
Winterthur, Switzerland

MFASIRI
Dkt. Gidion Kamfipo
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma

MSANIFU KURASA
Essy Ogunde
Creative Press Ltd

MSANIFU WA PICHA
Nuzulack J. Dausen
Nukta Africa

ISBN 978 99 87 710 70 6
Haki zote zimehifadhiwa.

Imetolewa na
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma
S.L.P 4067 Mikocheni B Makaburi Street, Plot Block D, No.34
Tel: +255 22 2700756 Dar es Salaam, Tanzania
Email: sjmc@udsm.ac.tz | yearbookmediatz@gmail.com

Yaliyomo

iii Shukrani
iv Muhtasari mahsusi
01 1.0 Utangulizi
03 2.0 Muktadha wa vyombo vya habari Tanzania
06 3.0 Muhtasari wa Matokeo
16 3.1 Magazeti
23 3.2 Redio
31 3.3 Televisheni
39 3.4 Hali ya uripoti wa vyombo vya habari Zanzibar
45 4.0 Maoni ya wadau
47 5.0 Hitimisho na mapendekezo
49 Viambatisho

Pakua ripoti zetu za nyuma
sjmc.udsm.ac.tz/yearbook/

Maudhui ya utafiti huu ni matokeo ya kazi ya utafiti iliyofanywa na watafiti wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (UDSM), na kwa namna yoyote ile hayawakilishi maoni ya Serikali ya Uswisi.

Shukrani

Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM-SJMC) inatoa shukrani za dhati kwa Ubalozi wa Uswisi na Uholanzi nchini Tanzania kwa kufadhili utafiti huu, na kwa jitihada zao endelevu za kuinua ubora wa vyombo vya habari na taaluma ya Uandishi wa Habari nchini.

Tunathamini na kuwashukuru wadau wa habari kwa utayari wao endelevu na kuunga mkono jitihada hizi zinazolenga kutafiti ubora wa maudhui ya vyombo vya habari nchini. Maoni yao kwenye warsha ya wahariri iliyolenga kupitia upya vigezo vya ubora vilivyotumika kwenye utafiti huu, utayari wao kusaidia wakati wa kurekodi kazi za kihabari na uwazi wao wakati wa mahojiano ni ishara tosha ya mchango wao uliotukuka katika kuunga mkono mradi huu wa utafiti.

Zaidi ya hapo, shukrani zetu za dhati zinaenda kwa Amidi wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma, Dkt. Mona Mwakalinga, kwa mwongozo wake wakati wa utafiti huu na Dkt. Gidion Kamfipo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuipitia ripoti hii. Vile vile tunapenda kutambua mchango wa watafiti wasaidizi hasa kwa namna walivyojitoa kufanikisha tafiti hii: Dianus Ishengoma, Vaileth Barden, Stanley Chungu, Gaspary Charles, Hamisi Kingu, Lameck Charles, Selemani Kodima, Yusuf Mohamed, David Lyimo, Theodora Munisi, Theodora Theodory, Caroline Malewo, Faidha Ngaga, Pascael George, Safina Yasini, Swaum Manengelo, Aisha Makame, Khalila Abdul Shaban, Shadida Salum, Adam Hhando, Lineth Renatus, Salma Tanzilu, Teddy Mparanyanga, Gertrude Mwambuba, Hafidhu Linguya and Amua Rushita.

Muhtasari mahsusi

Ubora wa uripoti wa kiuandishi wa habari nchini unaonesha muundo wa pande mbili. Upande mmoja, kuna ongezeko kubwa tu kwenye ubora kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na ubora uliopimwa mwaka 2019. Kwa aina zote za vyombo vya habari, uripoti kwenye vigezo vingi vya ubora umeimarika. Kwa mfano, uripoti wa vyanzo vingi vya habari, uripoti kuhusu mtazamo zaidi ya mmoja ndani ya habari na kufafanua vyanzo sababishi. Hata hivyo, kiwango cha uripoti bado kinahitaji maboresho zaidi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya maeneo yamebaki kwenye nafasi za chini: kuna kazi chache mno za kihabari zenye kubeba maoni kinzani (chini ya 2%), na kazi chache zinazoonesha ukosoaji kwa serikali (chini ya 4%).

Maendeleo chanya yamejitokeza zaidi kwenye habari na vipindi vya TV. Maeneo ya ubora yaliyoboreshwa kwa mwaka 2022 ni matumizi ya vyanzo vingi vya habari, uripoti wenye mitazamo mingi zaidi, na vyanzo sababishi kwenye habari na vipindi vya TV. Uripoti kwenye habari za redio umeimarika, lakini ni kwa kiwango cha chini kuliko ilivyo kwenye TV. Kwenye vipindi vya redio hali imebaki vilevile. Katika hali ya utofauti, magazeti yameonesha maendeleo chanya madogo, na katika baadhi ya vigezo vya ubora yamepata alama hasi. Inaonekana kwamba baadhi ya vituo vya TV na redio vimeboresha uripoti wao wa kihabari ilihali sekta ya magazeti imedumaa.

Kushuka kwa ubora wa uripoti kumesababishwa na hali ngumu ya kiuchumi inayovikumba vyombo vya habari, huku vikilazimika kuwa na watumishi wachache ambao wanafanya kazi zote. Kushindwa kuzingatia viwango vya uripoti kwa wahariri na waandishi nako kumechangia kushuka kwa ubora wa uripoti. Kiwango cha chini kabisa cha ujumuishaji wa maoni kinzani na habari zenye kumulika uwajibikaji wa serikali ni suala linalopaswa kutazamwa kwani vigezo hivyo viwili vya ubora vinaonekana kuwa muhimu kuwajengea uwezo hadhira wa kutoa maoni yao. Vigezo hivi vinaonekana kuwa vigumu kutekelezwa na vyombo vya habari nchini. Mpaka sasa vyombo vya habari ni kama bado havijarejea vizuri kwenye hali yake kutoka kwenye nyakati za shinikizo kali la kisiasa chini ya serikali iliyopita.

Huenda udumavu huu pia ukawa umechangiwa na uwezo mdogo wa waandishi wa habari na wahariri, kukamatwa kwa vyombo vya habari na wadau wenye maslahi yao kutoka serikalini, wanasiasa, na wafanya biashara na pengine hofu inayoendelea miongoni mwa wanahabari na hata vyanzo vya habari kuhusu kutoa maoni kosoaji kwa serikali. Kwa mujibu wa matokeo haya, tunashuhudia mabadiliko kwenye ubora wa uripoti. Baadhi ya vyombo vya habari vilivyokuwa vinaongoza mwaka 2019, mwaka 2022 vimejikuta mkiani kwenye msimamo wa ubora wa uripoti. Kwa mfano, baadhi ya redio za mikoani hazikufanya vizuri kama huko nyuma, hii ikiwa imechangiwa kwa kiasi fulani na changamoto za kiuchumi, ambazo zimesababisha baadhi ya waandishi kutafuta kazi nyingine zenye maslahi zaidi. Hali hii inaonekana kuwa changamoto sugu kwa vituo vidogo vya redio. Zaidi ya hapo, misaada kutoka kwa wafadhili imepungua, jambo ambalo linayafanya mazingira ya kiuchumi kuwa magumu zaidi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya vyombo vya habari, hata vile vinavyomilikiwa na serikali, vimefanya vizuri kuliko hata ilivyokuwa mwaka 2019, hasahasa kwenye maeneo ambayo siyo nyeti kwa serikali. Uripoti unaozingatia ujumuishaji wa mitazamo mingi zaidi, usuli wa kihistoria na vyanzo sababishi ni maeneo ya vigezo vya ubora yaliyoboreshwa.

Ikilinganishwa na mwaka 2019, changamoto ya kujiendesha kibiashara imekuwa hoja ya msingi ambayo huathiri ubora kwa haraka sana. Ingawa baadhi ya wadau wanaona kuna mabadiliko ya mazingira ya kisiasa nchini, ukilinganisha na huko nyuma, wengine hawana uhakika linapokuja suala la waandishi na vyanzo vya habari kuelezea maoni yao kwa uwazi. Hata hivyo, changamoto za ndani ya vyumba vya habari bado zinaendelea kuwa ni tatizo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma. Ukosefu wa mafunzo ya ndani kwenye vyumba vya habari bado unachangia kudumaza ubora wa uripoti, sambamba na kutofuatwa kwa miongozo ya kihariri na ukosefu wa utamaduni wa kujifunza. Tofauti na changamoto ya kibiashara, changamoto hizi za ndani zinaweza zikashughulikiwa kwa haraka zaidi na hivyo kuongeza mara moja viwango vya ubora.

Utangulizi

1.0 Utangulizi

Tangu kuzinduliwa kwa ripoti kamili ya Mradi wa Ubora wa Vyombo vya Habari Tanzania "*Yearbook on Media Quality in Tanzania*" mwaka 2018, tayari ripoti tatu zimeshachapishwa[1]. Ripoti zote tatu, zimeelezea kwa kina ubora wa uripoti wa habari nchini na kwa hiyo ripoti hizo zinaweza kutumika kama rejea pekee zilizopo kuhusu ubora wa uripoti wa habari nchini Tanzania. Ripoti ya mwaka huu imeendelea kuchunguza ubora wa uripoti kwa kuangalia aina tatu za vyombo vya habari – vinavyomilikiwa na serikali, vinavyomilikiwa na taasisi binafsi na vituo vya redio vya mikoani. Ili kurahisisha usomaji na kwa kuzingatia mahitaji ya wadau wa habari ambao ama wanafanya kazi kwenye kundi fulani la vyombo vya habari (redio, magazeti na televisheni), au wenye maslahi na kundi fulani la vyombo vya habari, ripoti hii imeyawasilisha matokeo ya utafiti katika sehemu nne: muhtasari unaotoa picha ya jumla ya matokeo ya utafiti, matokeo ya magazeti, redio na televisheni. Tofauti na ripoti zilizotangulia, ripoti hii imejumuisha sehemu mahsusi inayoangazia ubora wa uripoti wa habari visiwani Zanzibar. Ripoti kamili inapatikana kupitia ukurasa huu: (https://sjmc.udsm.ac.tz/yearbook/).

2.0 Muktadha wa vyombo vya habari Tanzania

Mpaka kufikia mwezi Aprili 2022, kulikuwa na vituo vya redio 210, vituo 56 vya huduma za utangazaji, na magazeti na majarida 284[2] kwa Tanzania bara[3]. Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)[4], hadi kufikia mwezi Agosti, 2020, idadi ya watoa huduma za maudhui mtandaoni ilikuwa 575. Watoa huduma za maudhui mtandaoni hujumuisha blogu za mtandaoni, majukwaa ya mtandaoni, redio za mtandaoni, Televisheni za mtandaoni, na huduma nyingine za mtandaoni. Umiliki wa maudhui mtandaoni unazihusu taasisi za kiserikali, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, makampuni, taasisi za mafunzo na utafiti na taasisi za kidini. Wamiliki wengi ni taasisi zisizokuwa za habari.

Tasnia ya habari Zanzibar pia inaendelea kukua. Kwa mujibu wa Tume ya Utangazaji Zanzibar (ZBC)[5], visiwani humo kuna zaidi ya taasisi 50 za utangazaji na huduma za habari mtandaoni ambazo tayari zimeshasajiliwa. Umiliki wa vyombo vya habari vya uchapishaji, kwa sehemu kubwa unatawaliwa na magazeti yanayomilikiwa na serikali—Zanzibar Leo, Zanzibar Mail, Zaspoti, na Zanzibar Leo Wanawake. Ni Fumba Times pekee, gazeti la mtandaoni lililoanzishwa Juni 2019[6] , ndilo gazeti binafsi linalochapishwa Zanzibar.

1 Ripoti ya majaribio ilichapishwa mwaka 2017

2 Idadi hiyo inajumuisha magazeti na majarida yote yaliyosajiliwa yanayomilikiwa na vyumba vya habari, taasisi za kiserikali, taasisi za kidini, taasisi za mafunzo, taasisi zisizokuwa za kiserikali, nakadhalika.

3 Hotuba ya bajeti ya wizara husika ya mwaka 2022/2023 inayopatikana kupitia: https://www.mawasiliano.go.tz/uploads/documents/sw-1653033707-Hotuba-Waziri-WHMTH%20bajeti%202022-23.pdf

4 Leseni za utoaji maudhui mtandaoni, zinazopatikana kupitia: https://www.tcra.go.tz/uploads/documents/en-1619022420-LICENSED%20ONLINE%20CONTENT%20SERVICES%20PROVIDERS%20AS%20AT%2025th%20AUGUST,%202020.pdf

5 website: https://tuz.go.tz/aboutus_link.php

6 Unaweza ukasoma toleo la kwanza kupitia kiunganishi hiki: https://fumba.town/wp-content/uploads/2020/06/FumbaTimes_01.pdf

WAMILIKI WAKUBWA WA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA

- Serikali ya Tanzania
- Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Aga Khan
- Dkt. Anthony Diallo
- IPP & Guardian Limited
- Familia ya Bakhresa
- Chama Cha Mapinduzi
- Joseph Kusaga

2.1 Sheria za habari na uhuru wa vyombo vya habari

Kuna sheria kadhaa zinazosimamia tasnia ya habari Tanzania bara, ikiwamo Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 ikiwa ndio sheria mama. Tangu kupitishwa kwa sheria hii, kuliibuka sauti nyingi na zinazoongezeka kwa kasi kutoka kwa wadau wa tasnia ya habari – wa ndani ya nchi na wa kimataifa – wakiipinga huku wakitoa wito wa kupitiwa upya kwa sheria hiyo. Sehemu ya wadau hao ni Baraza la Habari Tanzania (MCT), Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambao waliamua kutumia mkakati wa kisheria kuipinga sheria hiyo kwenye Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ) kwa misingi kwamba sheria hiyo inavunja misingi ya mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwenye hukumu yake, Mahakama ilibainisha wazi baadhi ya maeneo ya sheria hiyo yanayovunja misingi ya mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuielekeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuipitia upya sheria hiyo kwa kuzingatia mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.[7]

Tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani mwezi Machi, 2021, pameshuhudiwa maendeleo chanya kwa mazingira ya vyombo vya habari nchini. Hii ni pamoja na hali inayoendelea ya mapitio ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, kuondoa zuio kwa Televisheni za mtandaoni, kuondoa mahitaji ya leseni kwa redio na TV ambazo zimeshasajiliwa kurusha matangazo yao mtandaoni; kupunguza kwa asilimia hamsini ada ya mwaka ili kuweza kurusha mtandaoni habari na matukio yanayojiri duniani (Kutoka dola 432 hadi kufikia dola 216 za Kimarekani), kupitia upya kanuni za maudhui yaani Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) za mwaka 2018 na kuondoa zuio la uchapishaji wa magazeti manne—*Mwanahalisi, Mawio, Tanzania Daima na Mseto.*[8] Kuondolewa kwa zuio la uchapishaji wa magazeti hayo manne kulitafsiriwa na Shirirka la Kimataifa la Haki za Binadamu (Amnesty International) kama 'hatua chanya' huku Muungano wa Asasi za Kiraia Duniani (The global civil society alliance-CIVICUS) likiichukulia hatua hiyo kama 'hatua moja ya kuelekea kwenye mwelekeo sahihi', huku taasisi hizi mbili zikiitaka serikali kufanya zaidi ya hapo ili kuhakikisha panakuwa na uhuru wa habari chini.

Akitoa maoni yake kuhusu kuondolewa kwa zuio la uchapishaji wa gazeti, mhariri wa gazeti la Mawio Simon Mkina aliupongeza uamuzi wa

7 MCT (2020). East African Court of Justice Decision on Media Services Act 2016 and its implications. Available at: https://mct.or.tz/wp-content/uploads/2020/09/EACJ-Decision-on-Media-Services-Act-2016-and-its-implication.pdf

8 Ni Tanzania Daima pekee ambayo imerudi sokoni

serikali, akibainisha kwamba "ni muhimu kuhakikisha kwamba sauti zote zinasikika kwa kuruhusu vyombo vya habari vinavyounga mkono serikali kupewa nafasi sawa na vyombo vya habari vinavyoikosoa serikali. Utofauti wa vyombo vya habari ni jambo lenye umuhimu mkubwa."[9]

Viashiria chanya vilivyofanywa na serikali mpya kwa namna fulani vimeiweka nchi kwenye nafasi nzuri kiasi kwenye msimamo wa dunia kuhusu uhuru wa habari. Faharasa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari ya mwaka 2022[10] inayoandaliwa na shirika la waandishi wa habari wasiokuwa na mipaka (Reporters Without Borders) inaonesha kuwa Tanzania imepanda kwa nafasi moja kutoka 124 hadi 123. Hili linajitokeza baada ya mwendelezo wa kushuka kwa kasi kwenye msimamo huo tangu mwaka 2016 hadi 2020 ambapo nchi ilidondoka kwa karibu nafasi 53 ndani ya miaka mitano.

Zaidi ya hapo, Taasisi ya Habari Kusini mwa Afrika ofisi ya Tanzania (MISA-TAN), kwenye ripoti yake ya kikanda ya mwaka 2021 inakiri wazi kuwa mazingira ya habari nchini yameimarika tangu serikali ya awamu ya sita ilipoingia madarakani ikibainisha utayari wa serikali kukutana na wadau kujadili maboresho ya sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya habari nchini, kupungua kwa kiwango cha kuyafungia magazeti pamoja na kuvipiga faini vyombo vya habari vya utangazaji na watoa huduma za maudhui mitandaoni.[11]

Kufungiwa vyombo vya habari

Pamoja na kuimarika kwa mazingira ya vyombo vya habari nchini, mnamo tarehe 5 Septemba 2021, serikali ililifungia kwa muda wa mwezi mmoja gazeti la Raia Mwema kwa kile kilichosemekana kujirudiarudia kwa ukiukwaji wa sheria (sheria ambayo sasa inafanyiwa maboresho) na misingi ya taaluma ya uandishi wa habari kwa kuandika habari zenye upotoshaji na uchochezi.[12] Japokuwa Mhariri wa gazeti husika alipinga tuhuma hizo, lakini alikubaliana na amri hiyo.[13] Akizungumzia kusimamishwa kwa gazeti hilo, Mwakilishi wa Kamati ya Kuwalinda Waandishi wa Habari Kusini mwa Jangwa la Sahara (Committee to Protect Journalists (CPJ) Sub-Saharan Africa) Muthoki Mumo alidokeza, "ahadi za serikali ya Tanzania kuboresha mazingira ya uhuru wa vyombo vya habari nchini zitaendelea kushuka kwa kasi iwapo mamlaka zitaendelea na mwenendo wa kuyafungia magazeti kuonekana mitaani kwa visingizio visivyo na mashiko."[14]

Habari iliyomhusu Rais na kufungiwa kwa gazeti la chama tawala

Tarehe 11 Agosti, 2021, Uhuru gazeti la chama tawala (Chama Cha Mapinduzi-CCM) lilichapisha habari kuu kwenye ukurasa wa mbele iliyodaiwa kutokana na mahojiano ya Rais na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) iliyokuwa na kichwa cha habari "Sina wazo kuwania urais 2025 - Samia". Siku hiyo hiyo, serikali ililifungia gazeti hilo la chama kwa siku 14 kwa kuchapisha kile ilichokiita habari ya uwongo. Mkurugenzi wa Idara ya Habari–MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa alijitokeza na kutoa ufafanuzi kwamba Rais Samia Suluhu Hassan hakutoa tamko lolote kuhusu yeye kutogombea kwenye uchaguzi wa urais wa 2025. Gazeti hilo lililo sokoni tangu Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 pia lilifungiwa na mmiliki wake CCM kwa siku saba. Uongozi wa juu wa gazeti ulisimamishwa, na chama kiliunda kamati kuchunguza suala hilo. Mpaka leo, hakuna ripoti iliyotolewa kuhusiana na sakata hilo.

UHURU

Shaka awaumbua CHADEMA, ACT

Sina wazo kuwania urais 2025-Samia

Chongolo awataka wananchi kutunza miundombinu

9 MISA Tanzania welcomes lifting of ban on 4 newspapers, https://tanzania.misa.org/2022/02/10/misa-tanzania-welcomes-lifting-of-ban-on-4-newspapers/, retrieved on 16 September 2022

10 2022 Press Freedom Index, available at: https://rsf.org/en/index

11 2021 Regional Annual Report, https://data.misa.org/en/entity/r6wai83eb7b?utm_source=word%20press&page=1, retrieved on 12 August 2022

12 Leseni ya Gazeti la Raia Mwema yasitishwa kwa siku 30, https://twitter.com/MsigwaGerson/status/1434513147025571848, retrieved on 18th August 2022

13 Tanzanian authorities suspend Raia Mwema newspaper for 1 month, https://cpj.org/2021/09/tanzanian-authorities-suspend-raia-mwema-newspaper-for-1-month/, retrieved on 28 November 2022

14 Tanzanian authorities suspend Raia Mwema newspaper for 1 month, https://cpj.org/2021/09/tanzanian-authorities-suspend-raia-mwema-newspaper-for-1-month/, retrieved on 28 November 2022

Visiwani Zanzibar, Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Namba 7 ya Mwaka 1997 na Sheria namba 5 ya Usajili wa Mawakala wa Habari, Magazeti na Vitabu ya mwaka 1988 ndio sheria kuu zinazosimamia tasnia ya habari visiwani humo. Mwezi Machi, 2022, Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi alielekeza sheria hizo zifanyiwe mapitio ili kutengeneza mazingira rafiki kwa waandishi wa habari.[15]

2.2 Mazingira ya biashara ya vyombo vya habari

Kwa miaka sita iliyopita, mazingira ya biashara ya vyombo vya habari yamekuwa yakizorota kwa kiasi kikubwa, huku wahariri wakiguswa na kupungua kwa mapato yatokanayo na matangazo kwa kati ya asilimia 50-70.[16] Mlipuko wa UVIKO-19 uliifanya hali kuwa tete zaidi. Ripoti ya kitafiti iliyochapishwa hivi karibuni ya "State of the Newsroom in Tanzania: A survey report"[17] inabainisha kuwa vyombo vya habari nchini vilipitia changamoto ya kushuka kwa matangazo ya biashara kwa wastani wa asilimia 25.

Ripoti inabainisha zaidi kwamba, "kushuka kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara kulikuja na athari kubwa mno ikiwamo kuvilazimisha vyombo vya habari kupunguza wafanyakazi, kupunguza mishahara na kuwalazimisha wafanyakazi kuchukua likizo bila malipo" (Katunzi & Ssenabulya, 2022:14). Vyombo vingi vya habari bado havijatengemaa kutokana na mtikisiko huu.

Kwa ujumla, matangazo ya biashara ndio chanzo kikuu cha mapato kwa vyombo vya habari, kikifuatiwa na uuzaji wa vipindi. Kwa kutambua hatari ya kutegemea zaidi matangazo ya biashara kuwa chanzo kikuu cha mapato, baadhi ya vyombo vya habari vimeanza kutafuta vyanzo vipya vya mapato ambapo uandaaji wa matukio (outdoor events) unaonekana kushika hatamu.

Wakifafanua zaidi kuhusu suala hili la vyanzo vya mapato, Katunzi na Ssenabulya (2022) wanadokeza, "japokuwa ubunifu katika uandaaji wa matukio haya ya kujipatia kipato unatofautiana kati ya chumba cha habari na kingine kutegemeana na uwepo wa rasilimali fedha, imethibitika kuwa ni chanzo cha mapato kinachopendwa zaidi na vyombo vya habari. Changamoto pekee inayojitokeza kwenye uandaaji wa 'matukio' haya ni kwamba yanatumia muda na rasilimali nyingi kabla ya kupata umaarufu. Kwa hiyo, vyombo vya habari vinapaswa kuwa na uvumilivu wakati vikitafiti vyanzo mbadala vya mapato."

Uendeshaji endelevu wa kibiashara ni muhimu katika tasnia ya habari kama taasisi ya kibiashara na Mhimili wa Nne wa Serikali. Athari za vyombo vya habari kushindwa kufanya kazi zake kwa umahiri haziishii kwenye vyombo vya habari pekee, bali zinaathiri jamii nzima.

Panapokosekana vyombo vya habari vyenye tija, jamii siyo tu itakosa habari za kuaminika bali pia itakosa habari zinazokidhi viwango. Kudhoofika kwa vyombo vya habari kutokana na hali ngumu ya kifedha huviweka vyombo hivyo kwenye mazingira hatarishi ikiwemo uwezekano wa kutekwa na wanasiasa na watu wenye nguvu ambao mwisho wake huishia kuamua jinsi vyombo hivyo vinavyopaswa kuripoti habari zake. Hali hii ikitokea, huathiri namna habari mbalimbali zinavyoripotiwa ikiwemo habari za uvunjifu wa haki za binadamu, rushwa na utawala usio bora.

"Japokuwa ubunifu katika uandaaji wa matukio haya ya kujipatia kipato unatofautiana kati ya chumba cha habari na kingine kutegemeana na uwepo wa rasilimali fedha, imethibitika kuwa ni chanzo cha mapato kinachopendwa zaidi na vyombo vya habari."

15 Tanzania: Mwinyi Orders Sweeping Amendments of Zanzibar Media Laws, https://allafrica.com/stories/202203100703.html, retrieved August 2022

16 Katunzi, A., Spurk, C. (2020). Yearbook On Media Quality in Tanzania 2019, Dar es Salaam: University of Dar es Salaam' School of Journalism and Mass Communication (UDSM-SJMC)

17 Katunzi, A., Ssenabulya, B. (2022). State of the newsroom in Tanzania: A survey report, Kampala: African Centre for Media Excellence and National Endowment for Democracy

2.3 Wasifu wa waandishi wa habari Tanzania

Ili kuelewa ubora wa uripoti wa vyombo vya habari kwenye nchi fulani, ni muhimu kuliangalia suala hilo la ubora sambamba na wasifu wa wazalishaji wa kazi hizo – waandishi wa habari. Chati ifuatayo hapa chini inaonesha kwa ufupi matokeo ya utafiti wa hivi karibuni ambao uliangazia wasifu wa waandishi wa habari nchini Tanzania.

Wasifu wa mwandishi wa habari Tanzania



Chanzo: "A Portrait of Tanzanian journalists: A survey report, 2022"

Mkutano na wadau: Wawakilishi kutoka vyombo vya habari, taasisi za habari na serikalini wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya mkutano uliofanyika Dar es Salaam kupitia vigezo vya ubora vilivyotumika kwenye utafiti huu. Vigezo hivi vilipitishwa na wadau kwa mara ya kwanza mwaka 2017. Aliyesimama mstari wa mbele mwenye miwani ni Amidi wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma, Dr Mona Mwakalinga. **Picha na Glory Kavishe.**

3.0 MUHTASARI WA MATOKEO

Sehemu hii inatoa taswira ya matokeo ya utafiti huu na imegawanywa katika sehemu nne. Awali ya yote inatoa picha ya jumla ya matokeo yalivyo na baadae inaonesha matokeo mahsusi kuhusu magazeti, redio na televisheni na mwishoni inatoa picha ya matokeo yanayohusu uripoti wa vyombo vya habari visiwani Zanzibar. Kwa mwaka 2022, sampuli ilijumuisha kazi za kihabari 1887 ambazo ni habari na vipindi, kutoka kwenye magazeti tisa (9), vituo 15 vya redio (7 vya kitaifa na 8 vya kimkoa visivyokuwa vya kitaifa na vituo vitano (5) vya televisheni. Mbinu za utafiti huu zimeambatishwa mwishoni mwa ripoti hii.

Sampuli ya vyombo vya habari

Magazeti	Redio za Kitaifa	Redio za kimkoa	Televisheni
The Citizen	TBC Taifa	Dodoma FM	TBC 1
The Guardian	Radio Free Africa	CG FM	ITV
Mwananchi	Radio One	Highlands FM	UTV
Daily News	Clouds FM	Arusha 1 FM	STAR TV
Nipashe	Wasafi FM	Safari FM	ZBC TV
Jamhuri	EFM	Zenji FM	
Raia Mwema	ZBC Radio	Micheweni FM	
Habari Leo		Hits FM	
Zanzibar Leo			

Muktadha wa uripoti

Jitihada binafsi za vyombo vya habari kuripoti habari ambazo wamezitafuta wenyewe imeshuka kidogo ikilinganishwa na mwaka 2019 kwa wastani wa asilimia 2, na magazeti ndiyo yameporomoka zaidi kwa chini ya asilimia 5. Hii inamaanisha kwamba habari za matukio zimekuwa muhimu zaidi. Ni vipindi vya redio pekee ambavyo vimeonesha kufanya vizuri katika kigezo hiki (angalia sura inayohusu redio).

Muktadha wa uripoti wa habari

Aina ya chombo cha habari	Habari za matukio	Habari zisizo za matukio	Jumla
Magazeti	464	181	645
	72%	28%	100%
Redio za kitaifa	192	142	334
	58%	42%	100%
Redio za mikoani	237	237	478
	50%	50%	100%
Televisheni	170	151	321
	53%	47%	100%
Jumla	**1,063**	**711**	**1,774**
	60%	**40%**	**100%**

Hali ya uripoti kwa mada

Vyombo vya habari nchini huandika kuhusu mada mbalimbali. Masuala ya maendeleo (elimu, afya, kilimo, mazingira, maji) yameonesha kuripotiwa zaidi (asilimia 30), ikifuatiwa na masuala tete (migogoro, matatizo ya kijamii, rushwa, utawala bora, ukatili wa kijinsia kwa asilimia 25, na masuala ya kiuchumi (miundombinu, mafuta na gesi, ajira, biashara) asilimia 22. Masuala ya kisiasa yamepewa nafasi ndogo sana yakiwa na asilimia 10 ya uripoti wote, na masuala yanayohusu utafiti yameripotiwa kwa kiasi kidogo mno na vyombo vya habari (1%).

Vyombo vya habari vinaandika zaidi kuhusu maendeleo kwa kuwa ndio mada kuu inayobebwa na maofisa na viongozi wa serikali. Kwa kuwa uripoti wa vyombo vya habari kwa kiasi kikubwa unategemea taarifa rasmi zinazotolewa na viongozi hawa, hivyo, uwezekano wa masuala hayo kupewa kipaumbele na vyombo vya habari unakuwa mkubwa. Kwa upande mwingine, masuala ya kisiasa yameripotiwa kwa uchache kwa sababu kwa sasa pamekuwa na shughuli chache za kisiasa nchini. Hata hivyo, mijadala ya kisiasa imekuwa ya kudumu kwenye majukwaa ya mitandaoni kama vile *Twitter Space na Clubhouse.*

Mada zilizoripotiwa na vyombo vya habari



Uripoti wa Kimkoa

Dar es Salaam imekuwa ndio eneo la kijiografia lililoangaliwa na kuripotiwa zaidi likiwa na asilimia 20 ya uripoti, ikifuatiwa na Dodoma kutokana na dhima ya ukuaji iliyo nayo kama makao makuu ya nchi na makao makuu ya taasisi mbalimbali. Kama ilivyowahi kubainishwa kwenye ripoti zilizotangulia, mikoa yenye redio zake za ndani kwenye sampuli yetu imeonekana kuripotiwa zaidi ikilinganishwa na mikoa ambayo haina vituo vya namna hii. Ukweli huu unajibainisha *Arusha (Arusha One FM), Tabora (CG FM), Mbeya (Highlands FM),* Kaskazini Pemba (*Micheweni FM*), na Mwanza *(Radio Free Africa*). Mikoa iliyobaki imeripotiwa kwa uchache mno (chini ya asilimia 2).

Habari zinazotoka mijini na vijijini

Habari nyingi hazijaandikwa kwa mtazamo wa mada fulani inayoangazia eneo fulani kijiografia. Kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini, magazeti mengi yanachapisha habari nyingi ambazo si mahsusi kwa maeneo ya mjini au vijijini. Redio za ndani ya mikoa zina habari nyingi zinazohusu maeneo ya vijijini, lakini nyingi ya habari hizo zinaripoti kuhusu majiji muhimu kama vile Arusha, Dodoma, Mwanza, na Mbeya.

Mchanganuo wa habari zinazotoka mijini na vijijini

	Mjini	Vijijini	Mchanganyiko	Sio mjini wala vijijini	Jumla
Magazeti	139	115	10	427	691
	20%	17%	1%	62%	100%
Redio za kitaifa	144	52	5	147	348
	41%	15%	1%	42%	100%
Redio za mikoani	175	159	14	147	495
	35%	32%	3%	30%	100%
Televisheni	103	83	8	135	329
	31%	25%	2%	41%	100%
Jumla	561	409	37	856	1863
	30%	22%	2%	46%	100%

Habari za kitaifa au za kimkoa

Redio nyingi, kama vile *CG FM, Dodoma FM, Arusha FM, Safari FM,* na *Micheweni FM,* zinalenga maeneo husika na si kitaifa. Vyombo vya utangazaji vyenye leseni za kitaifa huwa wanaelekeza uripoti wao kwenye masuala ya kitaifa. Kwa ujumla, vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali visiwani Zanzibar vimechagua mwelekeo wa kuripoti masuala ya kitaifa (69% kwa *ZBC TV na 68% kwa ZBC Radio*). Hata hivyo, kwa Tanzania Bara, televisheni inavyomilikiwa na serikali, *TBC1,* imechangia kwa kiasi cha chini zaidi kwenye kuripoti habari za kitaifa (40%) ikilinganishwa na vyombo vingine vya habari vinavyomilikiwa na serikali na vituo vingine vikubwa vya redio binafsi za kitaifa.

Umuhimu wa habari za kitaifa

	Asilimia ya habari za kitaifa
ZBC TV	69%
ZBC Radio	68%
TBC Taifa	60%
Wasafi FM	58%
EFM	54%
TBC1	40%

Ubora wa habari kwa ujumla

Kipimo cha ubora

Kipimo cha ubora wa vyombo vya habari kinawasilisha muhtasari wa uripoti wa vyombo vya habari kwa kuzingatia maeneo tofauti ya ubora katika kipimo kimoja. Kiwango cha wastani cha ubora kimeimarika kutoka asilimia 27 mwaka 2019 hadi asilimia 32 mwaka 2022. Vyombo vya habari vilivyoongoza kwa mwaka 2022, kwa misingi ya viashiria tisa, ni *Jamhuri, Radio Free Africa, Mwananchi, Clouds FM na TBC Taifa.* Ikilinganishwa na mwaka 2019, magazeti ya Jamhuri na Mwananchi yameendelea kuwa kwenye nafasi zao za awali kwa kuwa miongoni mwa vyombo vitano bora vya habari nchini. Kwa upande mwingine, *Radio Free Africa, TBC Taifa na Clouds FM* vimeimarika mno ikilinganishwa na huko nyuma ambapo vyote viwili vilikuwa mkiani kwenye orodha ya 2019. Zaidi ya hapo, baadhi ya redio za kimikoa zimeshuka katika orodha hiyo.

Kipimo cha ubora, 2022



Vipimo vya ubora wa vyombo vya habari vinatoa picha ya jumla ya uripoti miongoni mwa vyombo vya habari nchini. Hata hivyo, kwa kuwa kipimo hukokotolewa kwa kutumia vigezo mahsusi vya ubora na kwa kutambua kwamba baadhi ya vyombo vya habari hufanya vizuri katika maeneo fulani fulani kuliko mengine, tulikokotoa ubora wa uripoti ili kupata vyombo vitatu bora vya habari kwa kila kigezo. Jedwali lifuatalo linatoa picha halisi.

Vyombo vitatu bora kwa kila kigezo cha ubora

Habari zisizo za matukio		Vyanzo vingi vya habari		Mitazamo miwili au zaidi ndani ya habari	
CG FM	74%	Micheweni FM	93%	Radio Free Africa	54%
Dodoma FM	72%	ZBC TV	84%	STAR TV	53%
Clouds FM	70%	TBC One	80%	Radio One	37%
Maoni ndani ya habari		**Ukosoaji kwa serikali**		**Vyanzo sababishi vya habari**	
Daily News	30%	Zenji FM	16%	Mwananchi	52%
The Citizen	29%	Radio Free Africa	15%	UTV	52%
Jamhuri	16%	Radio One	14%	Jamhuri	49%
Muundo mzuri sana wa uandishi		**Ujumuishaji wa usuli wa kihistoria kwenye habari**		**Utoaji haki ya kujibu tuhuma kwa watuhumiwa**	
TBC Taifa	100%	TBC Taifa	31%	Jamhuri	77%
Arusha 1 FM	100%	Jamhuri	29%	Mwananchi	60%
ZBC Radio	100%	TBC One	26%	Radio Free Africa	57%

Kwa ujumla, ubora wa uripoti unabainisha picha mbalimbali. Kwenye baadhi ya maeneo umeimarika (mfano kwenye vyanzo sababishi), lakini katika maeneo mengine umezorota kama kwenye ujumuishaji wa maoni ndani ya habari.kwa mfano, utofauti wa mitazamo na idadi ya maoni, vyote viwili vinaashiria udhaifu mahsusi. Uchache wa maoni kwa kiasi fulani unahusishwa na uwezo mdogo wa waandishi kwenye vyombo vingi vya habari.[20]

Muhtasari wa matokeo kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na 2019

Aina ya chombo cha habari	Vyombo vyote vya habari		Redio				Televisheni				Magazeti	
			Habari		Vipindi		Habari		Vipindi		Habari	Vipindi
Mwaka	**2022**	**2019**	**2022**	**2019**	**2022**	**2019**	**2022**	**2019**	**2022**	**2019**	**2022**	**2019**
Uripoti kimuktadha	40%	42%	19%	28%	95%	73%	10%	13%	94%	96%	28%	33%
Badiliko kwa 2022	▼ -2%		▼ -9%		▲ +22%		▼ -3%		▼ -2%		▼ -5%	
Vyanzo vingi vya habari	66%	60%	57%	49%	65%	66%	81%	57%	61%	55%	71%	68%
Badiliko kwa 2022	▲ +6%		▲ +8%		▼ -1%		▲ +34%		▲ +6%		▲ +3%	
Maoni	19%	15%	10%	5%	42%	33%	20%	5%	30%	28%	14%	13%
Badiliko kwa 2022	▲ +4%		▲ +5%		▲ +9%		▲ +15%		▲ +2%		▲ +1%	
Mitazamo	14%	7%	10%	4%	29%	12%	22%	1%	25%	8%	5%	5%
Badiliko kwa 2022	▲ +7%		▲ +6%		▲ +17%		▲ +21%		▲ +17%		▲▼ +/-0%	
Vyanzo sababishi	28%	24%	11%	12%	42%	33%	18%	6%	57%	53%	14%	13%
Badiliko kwa 2022	▲ +4%		▼ -1%		▲ +9%		▲ +12%		▲ +4%		▲ +1%	
Maoni kinzani	1.7%	2.8%	0.4%	1.1%	6.1%	3.7%	2.1%	1.2%	1.5%	2.8%	1.9%	2.4%
Badiliko kwa 2022	▼ -1.1%		▼ -0.7%		▲ +2.4%		▲ +0.9%		▼ -1.3%		▼ -0.5%	
Ukosoaji kwa serikali	3.9%	3.5%	4.5%	0.5%	3.4%	1.2%	2.7%	0.0%	3.8%	0.9%	4.1%	3.7%
Badiliko kwa 2022	▲ +0.4%		▲ +4%		▲ +2.2%		▲ +2.7%		▲ +2.9%		▲ +0.4%	
Haki ya kujibu	40%	25%	33%	6%	42%	33%	50%	23%	20%	100%	48%	27%
Badiliko kwa 2022	▲ +15%		▲ +27%		▲ +9%		▲ +27%		▼ -80%		▲ +21%	

20 Mahojiano na wahariri kuhusu hali ya uripoti wa habari.

Matokeo kwa kina

Vyanzo vingi vya habari

Suala la vyombo vya habari kutumia vyanzo vingi vya habari (vyanzo viwili au zaidi) limeimarika kwa asilimia 6 hadi kufikia asilimia 66. Theluthi mbili ya kazi zilizochunguzwa zimekidhi hitaji hili. Kuhusiana na aina ya vyombo vya habari, redio za kitaifa zimekuwa na uripoti wa chini kabisa zikipata asilimia 56 tu kwenye kazi zilizokuwa na vyanzo 2 vya habari au zaidi.

Vyanzo vingi vya habari

	0 au chanzo 1	vyanzo 2 au zaidi	Jumla
Magazeti	206	498	704
	29%	71%	100%
Redio za kitaifa	154	196	350
	44%	56%	100%
Redio za kimkoa	188	312	500
	38%	62%	100%
Televisheni	90	243	333
	27%	73%	100%
Jumla	638	1249	1887
	34%	66%	100%

Wanawake kama vyanzo vya habari

Ujumuishaji wa wanawake kama vyanzo vya habari ni suala muhimu kwenye uripoti wa habari kwani unatuhakikishia ujumuishi wa kijinsia. Kwa ujumla, aina zote za vyombo vya habari vimeboresha suala hili kwa kuwa na angalau mwanamke mmoja kama chanzo cha habari kwenye uripoti wao, kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

Ujumuishaji wa wanawake kama vyanzo vya habari

	Magazeti	Redio	Televisheni
2018	32%	43%	32%
2019	30%	36%	32%
2022	39%	44%	44%

Mitazamo

Kwenye kigezo hiki cha ubora, waandishi wa habari wanatarajiwa kutumia jicho mahsusi kwenye kushughulikia mada mahsusi. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mara nyingi vyombo vya habari nchini hutumia mtazamo wa kawaida wa kuliangalia jambo, hii humaanisha kwamba, wanaripoti habari zao kwa jicho la wananchi wa kawaida katika jamii. Mtazamo mwingine unaotumiwa mara nyingi ni mtazamo wa kiuchumi, jambo linaloonekana kuwa ni la dhahiri sana ikizingatiwa umuhimu wa masuala ya kiuchumi kwenye uripoti. Mtazamo wa kisiasa, si tu wanasiasa bali mvutano baina ya wadau mbalimbali unaonekana kuwa chini, wakati mtazamo wa sera unatumika zaidi. Mtazamo wa kisayansi unaonekana kutumika kidogo mno, kama ilivyo kwa mtazamo wa kiusalama.

Mitazamo kwenye uripoti	
Mitazamo	**Asilimia ya kazi zilizochunguzwa zenye mtazamo husika**
Habari zilizobeba mtazamo wa watu wa kawaida	41%
Mtazamo wa kiuchumi	19%
Mtazamo wa dola, sera na masuala ya kisheria	12%
Mtazamo wa siasa	6%
Mtazamo wa kiusalama	4%
Mtazamo wa kisayansi	1%
Mitazamo mingine	18%

Tukitofautishaji kati ya aina za vyombo vya habari, magazeti hupendelea zaidi kutumia mtazamo wa siasa kwenye uripoti wake kuliko mtazamo unaowahusu watu wa kawaida. Mtazamo wa sera hutumika zaidi na televisheni na magazeti, huku mtazamo wa kiuchumi ukiwa unatumiwa na aina zote hizi za habari. Habari yenye mitazamo mingi ni nzuri zaidi kwani inatumia mitazamo hiyo tofauti kulichunguza jambo moja. Kwa kutambua ukweli huu, utafiti huu umechambua idadi ya mitazamo kwenye kila kazi iliyochunguzwa kwa kuangazia vigezo vidogo vitatu: kazi zisizokuwa na mtazamo, kazi zenye mtazamo mmoja, na kazi zenye mitazamo miwili au zaidi. Chati ifuatayo inawasilisha matokeo kwa muhtasari.

Idadi ya mitazamo kwenye vyombo vyote vya habari



Maoni ndani ya habari

Hapa tunarejelea maoni ambayo yanatolewa na chanzo cha habari na ni lazima yaoneshe mwelekeo wa kimaamuzi ama yawe hasi au chanya. Kama ilivyo kwenye mitazamo hapo juu, maoni ya aina mbali mbali yana uwezekano mkubwa wa kutoa mwanga kwa hadhira ya vyombo vya habari na hivyo kuchochea mijadala ya umma. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa vyombo vya habari vilichapisha habari chache zenye kubeba maoni kamili ikilinganishwa na miaka iliyopita. Asilimia 66 ya kazi zilizochunguzwa hazikuwa na maoni kamili. Vile vile, idadi ya kazi zenye maoni 2 au zaidi kwa mwaka 2022 imeshuka.

Idadi ya maoni	
Idadi ya maoni	**Asilimia ya kazi zilizochunguzwa**
Hakuna maoni yaliyochukuliwa	76%
Maoni ya aina moja	14%
Maoni ya aina mbili	8%
Maoni ya aina tatu au zaidi	3%

N= 1502

Maoni kinzani

Uandishi mzuri wa habari unataka uchapishaji habari unaozingatia usawa. Hili linajumuisha uwasilishaji wa maoni kinzani ili hadhira iweze kujua upande mwingine wa habari husika. Kufanya hivyo kunahakikisha kuwepo kwa tafakari yenye usawa kwenye masuala yanayoripotiwa. Habari zenye maoni kinzani zimeonekana kuwa chache. Kwa wastani, asilimia ya maoni kinzani ilikuwa 1.7 tu, ambapo ni chini ya asilimia 2.8 ya mwaka 2019.

Maoni kinzani				
Idadi ya maoni	**Maoni yanayounga mkono upande mmoja**	**Maoni yanayokinzana**	**Maoni yanayokinzana**	**Jumla**
Magazeti	91	6	592	689
	13.2%	0.9%	85.9%	100%
Redio	155	20	651	826
	18.8%	2.4%	78.8%	100%
Televisheni	71	6	243	320
	22.2%	1.9%	75.9%	100%
Wastani	317	32	1486	1835
	17.3%	1.7%	81%	100%

Magazeti na vituo vya redio ambavyo huko nyuma viliwahi kuwa na kazi fulani ambazo zilikuwa na maoni kinzani, kwenye utafiti huu vimefanya vibaya kwenye kigezo hiki cha bora. Ni Clouds FM pekee yenye matokeo chanya ikionesha kuwa na angalau asilimia 30 ya kazi zenye maoni kinzani.

Maoni yenye ukosoaji

Vyombo vya habari vinapaswa kulinda utawala bora na kufuatilia uwajibikaji wa umma. Namna mojawapo ya kulitekeleza hili ni kutoa maoni yanayokosoa watendaji mbalimbali ndani ya jamii. Tofauti na ripoti zilizotangulia ambazo zililiangazia suala la maoni yenye ukosoaji kwa serikali tu, uchambuzi wa mwaka huu unakwenda zaidi ya hapo mpaka kwa wadau wengine kama vile sekta binafsi, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, taasisi za kidini na mengineyo. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba ni asilimia 4 tu ya kazi zote za kihabari zilizochunguzwa ndizo zilizotoa maoni kosoaji kwa serikali.

Maoni kosoaji		
	Idadi ya kazi	**Asilimia za kazi zote**
Ukosoaji kwa serikali	72	3.9%
Ukosoaji kwa sekta binafsi	9	0.5%
Ukosoaji kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali	13	0.7%
Ukosoaji kwa taasisi za kidini	10	0.5%
Ukosoaji kwa taasisi nyinginezo	43	2.3%
Jumla	**147**	1.6%

Ukosoaji kwa taasisi nyinginezo

Ukosoaji wa kina wa wadau wengine uko chini kuliko ule unaoelekezwa kwa serikali. Inavyoonekana, vyombo vya habari nchini havijazoea au havina uwezo wa kukosoa au kubainisha vyanzo vya habari vinavyochukua mkondo wa maoni kosoaji. Kwa mfano, vyombo vingi vya habari havikuchapisha maoni kosoaji dhidi ya sekta binafsi, isipokuwa vichache vilivyofanya hivyo mara moja tu. Hata hivyo, kuna masuala mengi yanayopaswa kuhojiwa ndani ya sekta binafsi.

Vyanzo sababishi vya habari

Kwenye uandishi wa habari, uripoti wa vyanzo sababishi vya habari ni eneo muhimu. Inafafanua chanzo sababishi cha tatizo au suala lililoripotiwa na si chanzo kingine chochote kuhusu kitu kingine. Inapaswa ihusiane na msingi wa habari iyoripotiwa. Hili linawawezesha waandishi wa habari kulihusisha suala linaloripotiwa na chanzo chake sababishi na hivyo, kutoa mchango chanya kwa uelewa wa hadhira kuhusu habari iliyoripotiwa. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba asilimia 28 tu ya kazi zilizochambuliwa ndizo zilizoripoti vyanzo sababishi vya habari husika. Hali hii imeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019 na 2018 ambapo uripoti kwenye eneo hili ilikuwa asilimia 24. Ikilinganishwa na mwaka 2019, magazeti na televisheni yameonesha maboresho makubwa kwenye kuripoti vyanzo sababishi (asilimia 33 na asilimia 34 dhidi ya asilimia 27 na 25 mwaka 2019), ilihali redio zimebaki kwenye nafasi za chini (22%).

Uripoti wa vyanzo sababishi

Aina ya chombo cha habari	Hakuna vyanzo sababishi	Vyanzo sababishi vichache	Vyanzo sababishi vingi	Jumla
Magazeti	250	209	229	688
	36%	30%	33%	100%
Redio	338	308	180	826
	41%	37%	22%	100%
Televisheni	94	117	109	320
	29%	37%	34%	100%
Wastani	**682**	**634**	**518**	**1,834**
	37%	**35%**	**28%**	**100%**

Usuli wa kihistoria ndani ya habari

Kwa ujumla, ujumuishaji wa usuli ndani ya kazi za kihabari uliripotiwa kwa asilimia 13 ya kazi zote zilizochunguzwa ikiwa ni ongezeko dogo kwa asilimia 2 ikilinganishwa na mwaka 2019. Vipindi vya redio na televisheni vimeripoti zaidi suala hilo kuliko ilivyokuwa kwenye habari (asilimia 2 kwenye redio, asilimia 5 kwenye televisheni). Magazeti yakiwa na asilimia 12 yameonesha kushuka kidogo (chini kwa asilimia 3). Hii inathibitisha matokeo ya tafiti za nyuma ambapo ujumuishaji wa usuli wa kihistoria ndani ya habari ulikuwa chini.

Uripoti wa usuli wa habari

	Hakuna usuli	Usuli kwa uchache	Usuli kwa wingi	Jumla
Magazeti	544	62	82	688
	79%	9%	12%	100%
Habari za Redio	479	43	11	533
	90%	8%	2%	100%
Vipindi vya redio	168	35	90	293
	57%	12%	31%	100%
Habari za televisheni	145	34	9	188
	77%	18%	5%	100%
Vipindi vya televisheni	75	13	44	132
	57%	10%	33%	100%
Wastani	1411	187	236	1834
Jumla	77%	10%	13%	100%

Haki ya kujibu tuhuma

Haki ya kujibu tuhuma ilibainika tu katika asilimia 40 ya kazi zote zilizochambuliwa. Hata hivyo, bado ni kiwango cha chini japo kuna maboresho chanya ikilinganishwa na mwaka 2019. Magazeti yamefanya vizuri (48%) kuliko redio na TV (karibu 33%).

Haki ya kujibu tuhuma

Aina ya chombo cha habari	Hapana	Ndiyo	Jumla
Magazeti	23	21	44
	52%	48%	100%
Redio	40	21	61
	66%	34%	100%
Televisheni	6	3	9
	67%	33%	100%
Wastani	**69**	**45**	**114**
	60%	**40%**	**100%**

Muundo wa uandishi kwenye habari

Idadi kubwa ya kazi (68%) zilikuwa na muundo mzuri sana wa kiuandishi, hali hii imeimarika zaidi kwa asilimia 14 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2019. Magazeti yaliboreshwa sana ikilinganishwa na mwaka 2019, kwa asilimia 30. Habari za kwenye redio na televisheni zilipata alama za chini kwenye kipengele hiki. Muundo wa kiuandishi kwenye vipindi umekuwa bora zaidi kwa asilimia (80%) ikiyakaribia magazeti (77%).

Muundo wa uandishi kwenye habari



3.1 MAGAZETI

Muktadha wa uripoti

Uripoti wa habari zinazotafutwa na vyombo vya habari vyenyewe, ambazo sio za matukio, umeshuka kwa asilimia 2 ikilinganishwa na mwaka 2019 (kutoka 42% hadi 40%). Kwa upande wa magazeti, hali hii ya kushuka ilikuwa mbaya zaidi (chini ya asilimia 5). Tofauti miongoni mwa magazeti ilikuwa kubwa. Magazeti ya serikali (Daily News, Habari Leo, Zanzibar Leo) yanaripoti zaidi habari za matukio (80% hadi 85%) kuliko magazeti binafsi kama vile Mwananchi na The Citizen (59% na 69%) au magazeti yanayotoka kila wiki (44% kwa Jamhuri, na 54% kwa Raia Mwema). Gazeti la The Guardian linaripoti zaidi habari za matukio kwa asilimia 87.

Nini huchochea uripoti kwenye magazeti?



Vyanzo vya habari

Kwa ujumla, magazeti yameboresha zaidi kazi zao kwenye kutumia vyanzo vingi vya habari (zaidi ya asilimia 3). Magazeti ya *Mwananchi na Daily News* yanaongoza kwa kuwa na kazi nyingi zilizotumia vyanzo vingi vya habari. Uripoti katika kigezo hiki cha ubora ni sawa na ilivyokuwa mwaka 2019 kwa magazeti mengi. Ni Habari Leo pekee ambalo limepata alama za chini (pungufu kwa asilimia 9) huku *Raia Mwema* likifanya vizuri zaidi (+33%).



Hata hivyo, utafiti ulibaini kazi 44 ambazo hazikuwa na chanzo cha habari ikiwa zimeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019 na 2018. Nusu ya kazi hizo (20) zikiwa ni za tahariri, maoni/uchambuzi, na nusu inayobakia ni habari na makala.

Wanawake kama vyanzo vya habari

Matumizi ya wanawake kama vyanzo vya habari ni moja kati ya vigezo muhimu vya ubora wa uandishi wa habari kwani husaidia sio tu kuleta uwiano wa kijinsia, bali kupaza sauti za wanawake. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kazi zilizokuwa na angalau mwanamke mmoja kama chanzo cha habari ziliongezeka kwa mwaka 2022, huku magazeti yakionesha ongezeko la asilimia 9.

Uripoti wa mada mbalimbali

Magazeti yanaonesha hali ile ile ambayo ripoti za nyuma zilibainisha. *Mwananchi* na *Raia Mwema* yanaripoti habari zenye mwelekeo wa kisiasa, huku *The Citizen* na *Daily News* yakiripoti masuala ya kiuchumi. Kwa ujumla, magazeti ya serikali na *The Guardian* yamejielekeza zaidi kwenye 'masuala ya maendeleo', huku Jamhuri na *Raia Mwema* huripoti zaidi mambo tete (rushwa, matatizo ya kijamii na utawala bora).

Uripoti wa mada

	Ajali/ Uhalifu	Maendeleo	Siasa	Uchumi	Utamaduni/ vyombo vya habari	Masuala yenye utata	Utafiti	Jumla
The Citizen	3	21	8	22	0	12	2	68
	4%	31%	12%	32%	0%	18%	3%	100%
The Guardian	2	25	6	18	0	10	2	63
	3%	40%	10%	29%	0%	16%	3%	100%
Mwananchi	10	18	13	11	2	16	1	71
	14%	25%	18%	16%	3%	23%	1%	100%
Daily News	2	12	5	32	1	21	0	73
	3%	16%	7%	44%	1%	29%	0%	100%
Nipashe	9	15	9	9	0	19	0	61
	15%	25%	15%	15%	0%	31%	0%	100%
Jamhuri	5	10	10	14	5	22	0	66
	8%	15%	15%	21%	8%	33%	0%	100%
Raia Mwema	5	12	15	9	5	23	0	69
	7%	17%	22%	13%	7%	33%	0%	100%
Habari Leo	3	20	6	21	4	10	0	64
	5%	31%	9%	33%	6%	16%	0%	100%
Zanzibar Leo	8	18	2	8	2	14	0	52
	15%	35%	4%	15%	4%	27%	0%	100%
Jumla	**47**	**151**	**74**	**144**	**19**	**147**	**5**	**587**
	8%	**26%**	**13%**	**25%**	**3%**	**25%**	**1%**	**100%**

Mitazamo ndani ya habari

Uripoti uliobeba mitazamo kwenye magazeti ni wa chini sana. Zaidi ya nusu ya kazi za magazeti (55%) hazikuwa na mitazamo, maana yake hayakuweza kuripoti au kufafanua masuala yaliyoripotiwa kwa kina. Ikilinganishwa na mwaka 2019, magazeti yamefanya vibaya, kwa sasa yakiwa na asilimia 15 zaidi ya kazi ambazo hazina mitazamo (55% dhidi ya 40%).

Magazeti: Idadi ya mitazamo



The Citizen, Jamhuri, na Mwananchi ndiyo yanafanya vizuri. Kwenye asilimia 55 hadi 60 ya kazi zake yanatoa angalau mtazamo mmoja, hali ambayo ni juu ya wastani. Ikilinganishwa na mwaka 2019, *Jamhuri* na *Daily news* zimebaki pale pale. *Nipashe:* limeshuka chini zaidi (59% hadi 34%); *Raia Mwema* limeshuka (kutoka 66% hadi 43%), *The Citizen* pia limeshuka (kutoka 74% hadi 55%), *Mwananchi* limeshuka (kutoka 61% hadi 55%), *The Guardian* limeshuka zaidi (kutoka 60% hadi 33%), *Habari Leo* limeshuka (kutoka 49% hadi 34%), na *Zanzibar Leo* (57% hadi 42%).

Maoni ndani ya habari

Kwenye utafiti huu magazeti yamekuwa na habari zenye kubeba maoni kamili kwa uchache ikilinganishwa na mwaka 2019. Asilimia ya kazi ambazo hazina maoni yoyote imeongezeka, hii sio hatua nzuri.

Uripoti wa maoni ndani ya habari

Asilimia ya "hakuna maoni kabisa"

Magazeti	2018	2019	2022	Badiliko
The Citizen	39%	59%	53%	▲ -5%
The Guardian	55%	70%	69%	▲ -1%
Mwananchi	29%	59%	76%	▼ +17%
Daily News	40%	81%	64%	▲ -15%
Nipashe	43%	77%	76%	▲ -1%
Jamhuri	31%	54%	70%	▼ +16%
Raia Mwema	-	63%	74%	▼ +11%
Habari Leo	-	83%	81%	▲ - 2%
Zanzibar Leo	41.30%	63%	81%	▼ +18%

Maoni kinzani

Kwenye magazeti, kazi zilizokuwa na maoni kinzani ni chache sana. Hata kwa yale magazeti yaliyokuwa na uripoti mzuri kwenye miaka iliyopita yameshindwa kuonesha japo kazi moja au mbili zenye maoni yenye usawa. Jambo hili linapaswa kupewa uzito mno kwenye vyumba vya habari. Kwa mwaka 2022, *The Guardian* lilikuwa na maoni yenye ukosoaji mkubwa kwa serikali, lakini kwa ujumla, uripoti wa magazeti uko sawa na ule wa mwaka 2019.

Magazeti: Maoni kosoaji kwa Serikali



Vyanzo sababishi vya habari

Matokeo ya utafiti yanaonesha picha tofauti kwenye uripoti wa vyanzo sababishi vya habari. Mwananchi linaongoza na kimsingi limeimarika (+20%), wakati *Jamhuri* (+26%) na *The Citizen* (+10%) yameongeza ubora wao. Magazeti ya serikali *Habari Leo, Daily News,* na *Zanzibar Leo* yameonesha kuwa chini kiasi katika kuripoti vyanzo sababishi vya habari, na *The Guardian* limekuwa la chini kabisa.



Usuli wa kihistoria ndani ya habari

Utofauti miongoni mwa vyombo vya habari unajibainisha wazi kwenye uripoti wa usuli wa kihistoria kwenye kazi zao. *Jamhuri* na *Mwananchi* yanaripoti zaidi usuli wa kihistoria wa jambo linaloripotiwa, yakifuatiwa na Raia Mwema. Kwenye kigezo hiki, magazeti yanayotoka kila wiki yanafanya vizuri zaidi.

Haki ya kujibu tuhuma

Ni vyombo vichache tu vya habari vilivyokuwa na idadi kubwa ya kazi ambazo zinatuhumu watu au taasisi, baadhi zikiwa na kazi moja au mbili hivi. Ukichukua magazeti yenye habari za aina hizi angalau 5 na zaidi, tunaona mambo yafuatayo:

- *Jamhuri* lilifanya vizuri likitoa nafasi ya kujibu tuhuma kwa wahusika kwenye kazi 10 kati ya 13 sawa na asilimia (77%).
- *Mwananchi* lilikuwa na 60% (kwenye kazi 3 kati ya 5)
- *Raia Mwema* lilikuwa 50% (3 kati ya 6), na
- *The Citizen* likiwa na 29% (2 kati ya 7).

Kipimo cha ubora kwenye magazeti

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, magazeti ya *Jamhuri* na *Mwananchi* yanaongoza kwenye kipimo cha ubora kwa magazeti yakifuatiwa na *Raia Mwema* na *The Citizen*.

3.2 REDIO

Table 2: Sub title be here

Muktadha wa upatikanaji habari

Kwenye Redio, kuna tofauti ya wazi kati ya habari na vipindi. Taarifa za habari zimetawaliwa na habari za matukio kati ya asilimia 90 hadi 100. Hata hivyo, hali ni tofauti kidogo kwa redio za *Dodoma FM, CG FM, Clouds FM* na *Hits FM* ambazo zinajitahidi kuleta uwiano kati ya habari za matukio na zile za kutafuta wao wenyewe.



Kwa upande wa vipindi vya redio, hali ni tofauti. Kwa wastani, asilimia 95 ya vipindi vya redio vilitokana na jitihada za vyombo vya habari vyenyewe. Asilimia hii ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na mwaka 2019 (ongezeko kutoka 73% hadi 95%). Utofauti pekee ulijitokeza kwa *Zenji FM* ambayo ilikuwa na asilimia 33 tu ya vipindi vinavyotokana na jitihada za vyombo vya habari vyenyewe.





Vyanzo vya habari

Kwa mwaka 2022, matumizi ya vyanzo vingi vya habari yameongezeka kwenye habari za redioni kutoka asilimia 49 hadi 57. *Micheweni FM* ndicho kituo cha redio kinachoongoza kwenye kuwa na vyanzo vya habari viwili au zaidi, kikifuatiwa na *Hits FM, Radio One, na Clouds FM. Zenji FM, Arusha 1 FM, Safari FM na Wasafi FM* vina alama za chini vikiwa na habari zenye angalau asilimia 50 ya vyanzo viwili au zaidi vya habari.

Vipindi vya redio: Visababishi vya habari kwa wingi



Kwenye vipindi vya redio, asilimia 65 ya kazi zilizochunguzwa zilikuwa na vyanzo viwili vya habari au zaidi. Hata hivyo, *Safari FM na Clouds FM* vilionesha kuwa na alama za chini (33%). Vyombo hivyo pia vilikuwa na vipindi vichache kwa sababu havikuzalisha aina ya vipindi ambavyo vinahitajika kwenye utafiti huu.[21] Ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2019, kwa mara nyingine tena *Micheweni FM* ni miongoni mwa vituo vya redio vinavyoongoza, ikiwa ni pamoja na *Dodoma FM na Zenji FM. CG FM, ZBC Radio* na *Arusha 1 FM* vimeonesha kuimarika. *TBC Taifa* (-23%) na *Radio Free Africa* (-25%) vimeonesha kupunguza ubora wao kwenye kipengele hiki. Tofauti na ilivyokuwa mwaka 2019, ambapo *Safari FM* ilikuwa miongoni mwa vituo vitatu bora vya redio vilivyofanya vizuri kwenye kigezo hiki cha ubora, safari hii imeporomoka hadi kuwa kituo kilichofanya vibaya zaidi.

Wanawake kama vyanzo vya habari

Vituo vya redio vimeboresha uripoti wao kwa asilimia nane (8) linapokuja suala la kuwatumia wanawake kama vyanzo vya habari. Redio za mikoani zimezizidi redio za kitaifa kwenye kuwatumia wanawake kama vyanzo vya habari.

Uripoti kwa maeneo chombo husika kilipo

Kigezo hiki cha ubora ni hitaji la msingi hasa kwa redio za mikoani. Kama redio hizi zitaandika kuhusu masuala ya kitaifa kama vile mfumuko wa bei au mikakati ya serikali, itakuwa ni muhimu kwa hadhira ya eneo husika kufahamu ni kwa namna gani habari hizi zinaathiri mazingira na jamii zao. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba redio nyingi za mikoani hazichakati habari za kitaifa kwa muktadha wa maeneo yao. Zinaripoti habari za kitaifa kama zilivyo—kama zinavyoripotiwa na redio za kitaifa. Hii ni changamoto kubwa ambayo wahariri wa redio hizo wanapaswa kuishughulikia kwa kuwa redio hizi zinalenga kusaidia hadhira maalumu, na hivyo kuwa na haja ya kuchakata habari zao kwa muktadha wa maeneo yao.

Mitazamo ndani ya habari

Vituo vya redio vimeimarika katika eneo hili kwa kuongeza kazi zenye mitazamo miwili kutoka asilimia 8 hadi 17. Kuna utofauti bayana kati ya habari na vipindi, jambo ambalo ni la kawaida kwani habari huwa ni fupi na kwa hiyo kutoa fursa chache kuripoti habari fulani kwa kina na kwa mitazamo mbalimbali. Chati ifuatayo hapa chini inaonesha kwamba vituo vingi vya redio havibebi mitazamo kwenye habari zake. Hata hivyo, baadhi ya vituo vya redio vimefanya vizuri kwenye kujumuisha angalau mtazamo mmoja kwenye habari zao. Vituo hivyo ni pamoja na *Radio One, Radio Free Africa, Zenji FM* na *Safari FM,* ambavyo mara kwa mara vimetoa mitazamo miwili ndani ya habari.

21 Ili kupata vipindi kutoka kwenye redio hizo, ilitulazimu kurekodi vipindi hata baada ya kipindi cha kukusanya sampuli kupita.

Habari za redio: Idadi ya mitazamo



Kwenye vipindi vya redio, matokeo yanaonesha picha tofauti. *TBC Taifa, EFM* na *Radio Free Africa* zimejumuisha mitazamo miwili kwenye karibu kila theluthi mbili ya vipindi vyake, zikifuatiwa na *Micheweni FM, Clouds FM* na *Zenji FM*. Nafasi ya chini imeshikwa na *ZBC Radio, Arusha 1 FM* na *Dodoma FM,* zikiwa na zaidi ya theluthi ya vipindi ambavyo havijajumuisha mtazamo wowote.

Vipindi vya redio: Idadi ya mitazamo



Maoni ndani ya kazi za kihabari

Kwenye redio, picha mbalimbali zimejitokeza kwenye ujumuishaji wa maoni ndani ya habari na vipindi. Vituo vichache vya redio vimeimarika kidogo (alama hasi ni chanya kwa sababu idadi ya kazi zisizokuwa na mtazamo wowote inazidi kupungua).

Ujumuishaji wa maoni kwenye Radio

	Idadi na asilimia ya kazi ambazo ‘‘hazina mtazamo wowote’’			
Redio	**2018**	**2019**	**2022**	**Badiliko**
TBC Taifa	75.6%	53.6%	53%	▲ -1%
Radio One	66.7%	46.9%	78%	▼ +31%
Clouds FM	74.6%	49.2%	100%	▼ +50%
Wasafi FM	-	-	79%	-
EFM	-	-	93%	-
Dodoma FM	62.5%	54.7%	78%	▼ +23%
CG FM	37.1%	71%	79%	▼ +8%
Highlands FM	51.9%	42.6%	90%	▼ +47%
Arusha 1 FM	60.8%	54.4%	74%	▼ +20%
Zenji FM	55.1%	65%	37%	▼ +2%
ZBC Radio	54.8%	68.9%	83%	▼ +14%
Micheweni FM	47.6%	60%	82%	▼ +22%
Safari FM	-	74.1%	77%	▼ +3%
Hits FM	-	-	72%	-

Kwa kuwa habari kwenye redio hubeba maoni machache kuliko vipindi, utafiti huu umeangazia zaidi vipindi.

Vipindi vya redio: Maoni mawili au zaidi



Kwa mujibu wa chati hapo juu, kwa wastani, asilimia 18 ya vipindi vya redio vilikuwa na maoni 2 au zaidi. Redio zilizofanya vizuri katika eneo hili ni *ZBC Radio, Hits FM* na *Micheweni FM,* wakati *CG FM* ilipata alama za chini mno, ikiwa na asilimia 4 tu. Hata kwenye vipindi, vituo vingi vya redio havikuweza kukusanya vyanzo tofauti vya habari vyenye maoni tofauti.

Maoni kinzani

Kuwapatia wasikilizaji maoni kinzani ni jambo linalofanyika kwa uchache sana kwenye vituo vya redio. Ni *Clouds FM* pekee imekuwa mfano chanya katika hili. Ni muhimu kwa vituo vya redio kujiimarisha kwenye eneo hili la ubora kwani linawasaidia wasikilizaji kutambua maoni tofauti yanayohusu jambo moja.

Maoni kosoaji kwa serikali

Baadhi ya vituo vya redio vilikuwa na maoni kosoaji kwa serikali mengi zaidi kuliko ilivyokuwa kwenye magazeti. *Zenji FM, Radio Free Africa* na *Radio One* zilipata alama za juu kwenye kipengele hiki. Kwa ulinganisho, ubora wa vituo vya redio umeimarika kutoka kuwa chini ya asilimia 1 mwaka 2019 hadi asilimia 4 mwaka 2022. Kwa upande mwingine, baadhi ya vituo vya redio vimeendelea kutokuwa na ukosoaji wowote kwa serikali (tazama 0% hapa chini).

Redio: Maoni kosoaji kwa Serikali



Vyanzo sababishi vya kazi za kihabari

Uripoti wa vyanzo sababishi uko juu kwenye vipindi vya redio (42%), na kuna maboresho makubwa kwenye vipindi vya redio (+10%) ikilinganishwa na mwaka 2019. Vile vile inaonesha uripoti wa vyanzo sababishi kwenye habari kuwa ni changamoto inayoendelea kwani ubora wake umebaki kuwa wa chini kama ilivyokuwa mwaka 2019 (karibu 11%). Tafiti zilizopita zilibainisha kwamba habari za redioni ni fupi, kutokana na mtindo huu, zinashindwa kuwajuza vizuri wasikilizaji wao. Matokeo haya yanaweza kuonekana kama wito wa kubadilisha mtindo wa habari za redioni ili ziwe ndefu kuliko ilivyo sasa.



Miongoni mwa vipindi vya redio[22], *EFM* na *CG FM* wanaongoza, wakifuatiwa na *Clouds FM* na *Radio Free Africa. Dodoma FM* inashika mkia.



*Micheweni FM (-35%), Radio One (-42%), na Dodoma FM (-35%) n*dio vituo vilivyo chini kabisa kwenye eneo hili ikilinganishwa na mwaka 2019. *EFM, CG GM (+30%), Clouds FM* (ni vipindi 9 tu, +60%) na *Radio Free Africa* (+29%)—vyote vikiwa na zaidi ya asilimia 50 ya vipindi vilivyojumuisha vyanzo sababishi vya habari husika.

Usuli wa kihistoria ndani ya habari

Kwenye vipindi vya redio, *TBC Taifa* kwa sehemu kubwa (83%) inajumuisha usuli wa kihistoria ndani ya habari, ilihali *Micheweni FM* na *CG FM* hawaoneshi kitu hicho kwenye vipindi vyao. Kushindwa kuripoti usuli wa kihistoria kwenye masuala yanayoripotiwa kunawanyima wasikilizaji nafasi ya kulielewa suala husika kwa mapana. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuwekeza kwenye kutafiti usuli wa kihistoria wa jambo linaloripotiwa.

22 Vipindi vya Safari FM viliondolewa kwa sababu kulikuwa na vipindi vitatu tu.

Haki ya kujibu tuhuma

Ni vituo vichache tu vya redio viliona umuhimu wa suala hili na kwamba linastahili kufanyiwa kazi. Vituo vilivyofanya vizuri (kwa kuzingatia vituo vya redio vilivyokuwa na vipindi angalau vitano vilivyotuhumu watu au taasisi) ni:

- *Radio Free Africa*, 8 kati ya matukio 14 (57%)
- *Clouds FM*, 2 kati ya matukio 5 (40%)
- *Zenji FM*, 5 kati ya matukio 14 (36%)
- *Radio One*, 4 kati ya matukio 16 (25%).

Kipimo cha ubora Redio 2022



3.3 TELEVISHENI

Muktadha wa uripoti

Kama ilivyo kwa habari za redioni, habari nyingi za kwenye televisheni nazo ni zao la 'ruzuku ya habari' — habari za matukio. Hii inajumuisha taarifa rasmi kutoka kwa maafisa habari, taarifa kwa vyombo vya habari, mikutano na waandishi wa habari, nakadhalika. Ukiiondoa *UTV*, ambayo ilikuwa na robo ya uripoti wake uliotokana na jitihada binafsi za chombo cha habari kutafuta habari (na sio kurusha habari za matukio), vituo vya televisheni vilivyobakia kwa sehemu kubwa vilitegemea habari za matukio. Kwa upande wa *Star TV* na *ZBC TV,* taarifa zao za habari zilisheheni habari za matukio kwa asilimia 100.

Habari za Televisheni: Visababishi vya uripoti



Kwa upande wa vipindi vya TV, vilizalishwa kutokana na jitihada binafsi za chombo cha habari na ni asilimia 6 tu ya vipindi hivyo ndivyo vilizalishwa kupitia matukio ya kihabari.



Vyanzo vya habari

Kwa wastani, asilimia 81 ya habari za kwenye TV zilitumia vyanzo vingi vya habari. Tofauti na taarifa fupi za habari redioni, taarifa za habari za TV ni ndefu na hivyo kuweza kujumuisha vyanzo 2 au zaidi vya habari kwenye habari zake. Hata hivyo, utofauti kwenye matumizi ya vyanzo vingi vya habari haufanani baina ya kituo kimoja cha TV na kingine. *TBC1* ilikuwa na asilimia 38 ya vyanzo hivyo (kwenye kazi zenye vyanzo viwili au zaidi vya habari) vingi vikitoka serikali kuu na kwenye mamlaka za serikali za mitaa, huku watu wa kawaida (25%) na wadau wa elimu (10%) wakijumuishwa. Sehemu kubwa ya vyanzo vya habari vya *ZBC TV* vilitoka serikalini (56%). Kwa upande mwingine, *ITV* na *UTV* vilikuwa na vyanzo vichache vya habari kutoka serikalini.



Hali kama hiyo ilibainika kwenye vipindi. *ZBC TV* ilikuwa na kazi nyingi zaidi zenye vyanzo vya habari '2 na zaidi' na sehemu kubwa ya vyanzo vyake vikitoka serikalini (37%), ilihali vyombo vingine ikiwamo *TBC1* vikiwa na vyanzo vya habari kutoka maeneo mbalimbali.

Vipindi vya Televisheni: Vyanzo viwili na zaidi



Wanawake kama vyanzo vya habari

Ujumuishaji wa wanawake kama vyanzo vya habari kwenye vituo vya TV umeimarika kwa asilimia 12. Hili linaonesha kwa uwazi kabisa kwamba waandishi wa habari wanazidi kuwa makini na masuala ya kijinsia kwenye uripoti wao, jambo ambalo ni la msingi mno katika kuimarisha upatikanaji wa aina mbalimbali za vyanzo vya habari kwenye vyombo vya habari.

Mitazamo ndani ya habari

Kwa ujumla, vituo vya TV vimeimarika katika ujumuishaji wa mitazamo tofauti ndani ya habari. Kuna kazi nyingi zaidi zilizokuwa na mitazamo 2 na zaidi (kutoka asilimia 4 na sasa asilimia 23). Hata hivyo, kuna utofauti mkubwa miongoni mwa vituo vya TV. Vituo vya Televisheni vinavyomilikiwa na serikali *ZBC TV na TBC1* viko upande wa chini, vikiwa na kazi chache tu zilizozingatia angalau mtazamo mmoja (28% na 39%) mutawalia, ilihali *UTV, ITV* na *STAR TV* viko sehemu nzuri vikiwa juu ya asilimia (80) kwa kazi zake kuripoti angalau mtazamo mmoja. Kwa hiyo, vituo hivi vitatu vinachangia kwenye matokeo "mazuri" ya vituo vya TV kwenye kigezo hiki cha ubora.

Habari za Televisheni: Idadi ya mitazamo



Vile vile, kwenye vipindi, Star TV inaongoza miongoni mwa vituo vya TV. Kwa mara nyingine tena, vituo vya utangazaji vya serikali vimebaki kuwa chini hata kwenye vipindi—pamoja na kuwa na uwanja mpana wa uripoti, TBC1 haitoi taarifa na ufafanuzi wa kina kwa mtazamo mahsusi kwenye zaidi ya asilimia 50 za vipindi vyake.

Vipindi vya Televisheni: Idadi ya mitazamo



Maoni ndani ya habari

Kwa ujumla, *ITV* imeonesha maendeleo chanya, ikipunguza asilimia ya kazi zake ambazo hazikuwa na maoni kamilifu ndani ya habari zake. *ZBC TV* imeporomoka mno lakini kwa sasa iko kwenye kiwango sawa na *TBC 1*. *Star TV* inaongoza kwa kuwa na habari ambazo hazina maoni kamilifu, na mara zote inatoa maoni ya aina moja, na si zaidi.

Maoni kwenye TV

Asilimia ya kazi zisizokuwa na maoni kabisa

TV	2018	2019	2022	Badiliko
TBC 1	54%	66%	71%	▼ +5%
ITV	51%	74%	68%	▲ -7%
AZAM TV/UTV	52%	75%	89%	▼ +14%
STAR TV	-	-	29%	-
ZBC TV	-	36%	77%	▼ +31%

Kwa wastani, ubora wa TV uko chini kwa asilimia 10. Grafu hapo chini inaonesha kwamba UTV ikiwa na asilimia 31 imeimarika mno mwaka 2022, kutoka asilimia 21 mwaka 2019, lakini ubora wa *TBC1 na ITV* umeshuka mno (kutoka asilimia 36 mwaka 2019 hadi asilimia 3, na kutoka asilimia 37 hadi asilimia 9). Itakumbukwa kwamba mwaka 2018, vituo vyote vya TV vilikuwa na mafanikio ya juu kwenye kigezo cha kuwa na maoni 2 au zaidi. Hili linaibua swali, ikiwa vituo vya TV vinakosa uwezo au utashi wa kukusanya vyanzo vingi vya habari vinavyoelezea maoni yao kwa uwazi. Hata hivyo, matokeo ya *UTV* yanabainisha kwamba katika muktadha huu, uripoti wa juu unawezekana.

Vipindi vya Televisheni: Maoni mawili au zaidi



Maoni kinzani

Maoni kinzani yanaonekana kwenye asilimia 2 ya kazi za kwenye TV zilizochunguzwa kitu ambacho kinabainisha ubora ulio chini. Vituo vyote vya TV vimekuwa na ubora wa chini: *UTV, ITV* na *Star TV* vilikuwa na kazi moja tu kwenye kigezo hiki, *TBC1* ilikuwa na tatu na *Star TV* haikuwa na kazi yoyote. Wakati watu zaidi na zaidi wanatumia TV angalau kwa maeneo ya mijini kama chanzo chao cha msingi cha kujipatia taarifa, kuna kila sababu kwa vituo vya TV kuimarisha uripoti unaojumuisha maoni kinzani—maoni ya pande mbili yanayokinzana.

Ukosoaji kwa serikali

Vituo vya TV havikuonesha ukosoaji kwa serikali kwa mwaka 2019. Kwa mwaka huu, kuna kazi chache zimerushwa ambazo zinasimamia uwajibikaji wa serikali kama inavyoonekana kwenye chati hapa chini.



Vyanzo sababishi vya habari

Uripoti wa vyanzo sababishi vya habari ni wa juu kwenye vipindi vya TV (57%) kuliko ilivyo kwenye habari (18%). Huku ni kuongezeka kwa ubora kwenye vipindi vya TV (+4%) ikilinganishwa na mwaka, 2019. Habari za kwenye TV pia zimeboreshwa mno (kutoka 6% hadi 18%). Uripoti kwenye vipindi vya TV kwenye kigezo hiki umeonekana kuwa wa chini kwa *TBC1*, ambapo kuna kushuka mno ikilinganishwa na mwaka 2019 (-54%). *ITV na ZBC TV* zimeimarika mno. *ZBC TV* ilipata zaidi (+62%). *UTV* iliendelea kubaki kileleni.

Faida kubwa iliyonayo UTV ni kwamba inajumuisha vyanzo sababishi hata kwenye habari zake za kwenye TV, kitu ambacho hakifanyiki kwenye vituo vingine vya TV. *UTV* imeimarika mno ikilinganishwa na mwaka 2019 (+36%), na vyombo vingine vimeendelea kubaki chini.





Usuli wa kihistoria ndani ya habari

UTV na Star TV mara kwa mara huripoti usuli wa kihistoria (zaidi ya 50% ya kazi zilizochunguzwa) kwenye vipindi vyao. ITV na ZBC TV viko chini kabisa (karibu 10%).

Haki ya kujibu tuhuma

Miongoni mwa vituo vya TV, ni Star TV tu iliyokuwa na angalau kazi (5) zilizokuwa na tuhuma dhidi ya watu binafsi au taasisi. Ilitoa haki ya kujibu tuhuma kwa wahusika kwenye kazi (2) kati ya (6) zilizochunguzwa (33%).

Kipimo cha ubora Televisheni 2022



Ubora wa vituo vya TV uko kwenye hali inayofanana. *Star TV* inaongoza kwenye kipimo cha ubora kwa ujumla ikiwa na asilimia 38, ikifuatiwa na *TBC1, UTV, ITV na ZBC TV*.

3.4 HALI YA URIPOTI WA VYOMBO VYA HABARI ZANZIBAR

Sura hii inaangazia ubora wa uripoti wa kiuandishi wa habari visiwani Zanzibar. Kipengele hiki kipya kwenye ripoti hii ni mapendekezo ya wadau wa habari visiwani humo. Kwa upande wa Zanzibar, sampuli 370 ya kazi za kihabari zilizochukuliwa kutoka kwenye vyombo (6) vya habari, ambavyo ni *Zanzibar Leo, Zenji FM, ZBC Radio, Micheweni FM, Hits FM na ZBC TV*.

Mada zilizoripotiwa

Kama ilivyo kwa Tanzania Bara, uripoti wa vyombo vya habari Zanzibar ulitoa kipaumbele kwa masuala ya kimaendeleo kama vile elimu, afya, kilimo, mazingira, na maji (31%), vikifuatiwa na masuala tete (migogoro, haki za binadamu, matatizo ya kijamii, rushwa, utawala bora 27%), na masuala ya kiuchumi (19%). Maeneo haya matatu ndiyo yameonekana kupendwa na vyombo vya habari. Pia yanaakisi nini viongozi wa kiserikali, ambao ndio vyanzo vikuu vya taarifa kwenye vyombo vya habari, wanaangazia. Kwa mara nyingine tena, kama ilivyo kwa wenzao wa Tanzania Bara, vyombo vya habari Zanzibar vimeupa uzito mdogo uripoti wa masuala ya kisiasa, jambo hili linaweza kuhusishwa na uwepo mdogo wa shughuli za kisiasa visiwani humo. Hata hivyo, majukwaa ya mitandaoni kama vile *Twitter Space na Clubhouse* yanaendesha mijadala kuhusu siasa za Zanzibar.

Zanzibar: Mada zilizoripotiwa



Uripoti mada maalumu: uchumi wa buluu

Tangu ilipoingia madarakani mwezi Desemba 2020, awamu ya 8 ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Raisi Dkt. Hussein Ali Mwinyi[23] imekuwa ikipigania uchumi wa buluu kama chachu ya ukuaji wa uchumi Zanzibar na maendeleo yake ya baadaye. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kupitia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, inautambua uchumi wa buluu – matumizi endelevu ya bahari na rasilimali za baharini kukuza maendeleo jumuishi – kama kipaumbele chake kwa miaka 28 ijayo.

Kutokana na umuhimu wa sekta hii kwa uchumi wa Zanzibar, ripoti hii imeangazia jinsi vyombo vya habari Zanzibar vilivyoripoti kuhusu sekta hii kwa kuangalia maeneo yafuatayo ya kipaumbele: uvuvi na ufugaji wa samaki, biashara ya baharini na miundombinu, nishati, utalii, usimamizi wa bahari, sera, na fedha[24]. Ili kuhakikisha maeneo yote au ya msingi ya uchumi wa buluu yanaguswa, kulikuwa na kipengele cha 'mada nyingine yoyote' ya uchumi wa buluu zaidi ya zilizotajwa hapo juu. Utafiti ulichunguza kazi ambazo zilirejelea uchumi wa buluu. Kazi yoyote ambayo haikurejelea wazi uchumi wa buluu ilichukuliwa kama haijaripoti kuhusu sekta hiyo.

Ikilinganishwa na vyombo vya habari vya Tanzania Bara, vyombo vya habari vya Zanzibar vimeripoti zaidi kuhusu uchumi wa buluu ingawa haikuwa mada kuu katika uripoti wao kwa ujumla. Vyombo vya habari vya Zanzibar vilitenga chini ya asilimia 10 ya uripoti wao kwa masuala ya uchumi ya buluu.

Uripoti wa uchumi wa buluu

Vyombo vya habari Zanzibar	Idadi ya kazi	Asilimia
Micheweni FM	5	9%
ZBC TV	6	9%
Zanzibar Leo	6	8%
Zenji FM	4	7%
ZBC Radio	2	5%

Ndani ya uripoti wa uchumi wa buluu, sekta ndogo ya uvuvi na ufugaji samaki (kazi 9 kati ya 23 kwa ujumla, 39%) ziliripotiwa zaidi, zikifuatiwa na utalii na miundombinu.

Visababishi vya uripoti

Kwa ujumla, habari za matukio ndizo zinazoongoza kwenye uripoti wa vyombo vya habari Zanzibar, vikiwa na asilimia 64 ya kazi zilizotokana na matukio. Zenji FM hutegemea zaidi habari zinazotokana na matukio kwa asilimia 88, ikifuatiwa na *Zanzibar Leo (83%) na ZBC Radio (68%).* Vyombo vya habari vya serikali vinaengemea zaidi habari zitokanazo na matukio kuliko vyombo binafsi vya habari, hii ni kwa sababu huripoti zaidi matukio yanayofanywa na viongozi wa serikali.

Zanzibar: Visababishi vya uripoti



23 Wakati wa kampeni za uchaguzi wa urais za mwaka 2020, Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliuweka uchumi wa buluu kama agenda kuu ya kampeni zake.

24 Sekta hizi ndogo zimetajwa kwenye Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2020.

Kwenye jitihada binafsi za chombo cha habari—habari zinazokusanywa na vyombo vyenyewe vya habari—*Hits FM* ina asilimia kubwa zaidi (64%), ikifuatiwa na *Micheweni FM* (53%). Hili ni jambo zuri kwani kuwa na kazi nyingi zaidi zinazozalishwa kwa jitihada zao binafsi sio tu huwasaidia wananchi kupata habari zenye usawa – habari za kawaida dhidi ya zisizo za kawaida, lakini pia huvisaidia vyombo vya habari kutengeneza ajenda zao na hivyo kuchangia majadiliano kwa umma.

Vyanzo vya habari

Kutumia vyanzo vingi vya habari, '2 au zaidi' ni jambo linaloonekana kueleweka kwa vyombo vya habari vya Zanzibar. *Micheweni FM* imevishinda vyombo vingine vyote kwenye eneo hili, huku asilimia 93 ya kazi zake zikiwa na vyanzo vya habari 2 au zaidi, ikifuatiwa na vyombo vinavyomilikiwa na serikali *ZBC TV* (84%) na *Zanzibar Leo* (76%). Vyombo hivi vitatu vya habari vimefanya vizuri zaidi ya alama ya wastani (74%).

Zanzibar: Vyanzo viwili au zaidi



Mitazamo ndani ya habari

Matokeo kwenye kutumia mitazamo au jicho mahsusi kwenye uripoti yanaonesha picha tofauti. *Zenji FM* na *Micheweni FM* zina kazi nyingi zaidi zenye mitazamo 2 na zaidi, zaidi ya hapo ni kazi chache tu ambazo zilikuwa 'hazina mtazamo wowote'. Hii humaanisha kwamba wanaripoti kwa kina na kutoa ufafanuzi wakichunguza kwa mtazamo mmoja au zaidi. Kwa upande mwingine, vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali havifanyi vizuri kwenye eneo hili vikiwa na zaidi ya nusu ya kazi zao zikiwa hazina jicho mahsusi ambalo kazi hizo huripotiwa kwalo

Zanzibar: Mitazamo kwenye habari/vipindi



Maoni ndani ya habari

Kuhusiana na ujumuishaji wa maoni kamilifu ndani ya habari, vyombo vya utangazaji vinavyomilikiwa na serikali bado vimeendelea kuwa na ubora wa chini kuliko vituo binafsi vya redio. Hivyo, *Zenji FM, Hits FM* na *Micheweni FM* hutoa maoni kamilifu mengi zaidi na hivyo kuwasaidia wasikilizaji kuhabarika zaidi.

Zanzibar: Maoni mawili au zaidi



Maoni kinzani

Maoni kinzani ni kama hayapo kabisa kwenye vyombo vya habari vya Zanzibar. Ni kazi tatu (3) tu kati ya 370 zilizobeba usawa na maoni kinzani, ikiwa ni sawa na asilimia 0.8. Hili humaanisha kwamba ama vyombo vya habari visiwani Zanzibar haviliangalii hili kuwa ni kazi yao au hawapati vyanzo vya habari vinavyoweza kutoa aina hii ya maoni.

Ukosoaji kwa serikali

Habari zinazosimamia uwajibikaji kwa serikali ni adimu kwenye vyombo vya habari Zanzibar. Ni asilimia 3.4 tu zikiwakilisha kazi 12 kati ya 370. *ZBC Radio, Hits FM na ZBC TV* havina hata kazi moja inayoangazia uwajibikaji wa serikali, na *Micheweni FM* ilikuwa na kazi moja tu. Udhaifu huu unawakosesha wananchi nafasi ya kutengeneza maoni yao kuhusu serikali na inadhoofisha imani ya wananchi kuhusu uhuru wa vyombo vya habari Zanzibar.

Zanzibar: Maoni kosoaji kwa Serikali



Usuli wa kihistoria ndani ya habari

Ujumuishaji wa usuli wa kihistoria kwenye habari limekuwa ni jambo adimu kwenye vyombo vya habari vya Zasnzibar (wastani 8%). Inaonekana kana kwamba aina hii ya taarifa za kina imekuwa ni changamoto kuitimiza. Vyombo vingi vya habari havioni haja ya kuwa nayo, au pengine waandishi wa habari wanakosa uwezo wa kutafuta vyanzo vya habari vitakavyozungumzia jinsi habari ilivyojitokeza hapo awali.

Vyanzo sababishi vya habari

Vyombo vya habari vyote viwili, *ZBC TV* na *Micheweni FM,* vilikuwa na kazi nyingi (38% na 35%) zinazowapa hadhira ufafanuzi wa vyanzo sababishi vya masuala yanayojitokeza kwenye habari hizo. Kwa upande mwingine, *Zenji FM* na *ZBC Radio* vimekuwa na ubora wa chini mno kwenye kigezo hiki cha ubora.

Zanzibar: Vyanzo sababishi vya habari



Muundo wa uandishi wa habari

Muundo wa habari unatofautiana mno miongoni mwa vyombo vya habari Zanzibar. *Zenji FM* na *Micheweni FM* vimeshika nafasi ya chini, chini zaidi ya wastani wa kuwa na muundo mzuri wa habari. *ZBC Radio, Hits FM* na Zanzibar Leo wamefanya vizuri katika eneo hili. Kuwa na muundo mzuri wa habari inasaidia hadhira, yaani wasomaji, wasikilizaji na watazamaji, kuifuatilia vizuri habari pasipo kupotea.



Haki ya kujibu tuhuma

Maadili ya taaluma ya uandishi wa habari yanataka kwamba mtuhumiwa yeyote lazima apewe haki ya kujibu tuhuma. Kwa kufanya hivyo, kunawapa watuhumiwa nafasi ya kutoa upande wao wa taarifa. Kwenye kigezo hiki cha ubora, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba *Zenji FM* ndio chombo pekee cha habari kilichokuwa na kazi nyingi (14) za watu waliotuhumiwa. Vyombo vingine vya habari vilikuwa na kazi nne (*Zanzibar Leo*) au habari moja (*Hits FM, ZBC TV*), na *ZBC Radio* haikuwa na habari yoyote ya aina hiyo. Kwa upande wa *Zenji FM,* imetoa haki ya kujibu tuhuma kwa watuhumiwa kwenye kazi 5 tu (= 36%).

Kipimo cha ubora kwa vyombo vya habari Zanzibar

Kipimo cha ubora kinatoa muhtasari wa utendaji wa vyombo vya habari kwenye aina tofauti za ubora ndani ya kipimo kimoja. Kiwango cha juu kabisa cha ubora kilifikiwa na *Hits FM,* ikifuatiwa na *Micheweni FM.*



4.0 MAONI YA WADAU

Sura hii inalenga kuweka wazi maoni ya wahariri na wadau kuhusu ubora wa uripoti nchini. Sehemu hii inatoa picha ya jumla ya changamoto zinazohusiana na ubora wa uripoti badala ya kuangalia maeneo mahsusi ya changamoto za uripoti. Kwa ujumla, kuna aina kuu mbili za changamoto—zile zitokazo ndani ya vyombo vya habari na zile zitokazo nje ya tasnia ya habari. Watu 10 walihojiwa, wakiwamo wahariri waandamizi 7, wawakilishi 2 kutoka kwenye taasisi zinazosaidia sekta ya habari na mkufunzi 1 wa uandishi wa habari.

Tofauti na ilivyokuwa kwenye ripoti zilizopita ambamo wahojiwa waliyataja mazingira ya kisiasa nchini kama shinikizo namba moja kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari nchini, mazungumzo na wahariri na wadau wa habari yanaonyesha kuwa mazingira magumu ya kisiasa yaliyokuwapo hapo nyuma kwa sasa yamekuwa nafuu. Mmoja wa wahariri waandamizi alielezea hali hii:

"...kwenye kipindi cha miaka ya nyuma, vyombo vya habari vilikuwa vikipewa maonyo kila viliporipoti kitu chochote kilichoonekana kuikosoa serikali. Kwa sasa sijasikia chombo chochote cha habari au mwandishi wa habari akionywa kwa sababu ya kile alichokiandika. Hata hivyo, kwa maoni yangu hili linatokana na utashi wa kisiasa wa serikali iliyoko madarakani, na si sheria zinazosimamia vyombo vya habari. Bado tuna sheria zile zile zilizokuwa zinaviadhibu vyombo vya habari, ikiwamo kuvifungia vyombo vya habari vilivyokuwa vinaikosoa serikali. Tunahitaji kuubadilisha mfumo wote uliopo wa sheria kandamizi ili kutoa fursa kwa vyombo vya habari kutekeleza majukumu yake kama Mhimili wa Nne wa Serikali."

Akiongezea kwenye suala hili, mhojiwa mwingine alidokeza kwamba mpaka leo baadhi ya wahariri hawana uhakika kama watasalimika ikiwa watachapisha habari zenye ukosoaji kwa serikali. "Unaona, uripoti mwingi unaangazia agenda ya serikali ya maendeleo au shughuli za wadau wengine, lakini hakuna uripoti wenye ukosoaji na wa kina. Sio kwamba hatuyaoni maeneo yanayohitaji uripoti wa kina, lakini ni kama tulikuwa kwenye chumba cha wagonjwa mahututi kwa muda mrefu na sasa tumerudishwa kwenye wodi za kawaida tukisubiri kuruhusiwa."
Ukosefu wa uripoti wa kina pia unahusishwa na kukataa kwa vyanzo vya habari kuelezea maoni yao kwenye habari zinazoonekana kama zinakosoa mamlaka. Akifafanua hili, mhariri mwandamizi alibainisha, "kuna mambo mawili hapa. Baadhi ya vyanzo vya habari hutujia na kutoa maoni yao kuhusu habari chanya kwa serikali au wako tayari kutoa maoni yao kuhusu habari hizo wakasikika. Hata hivyo ikiwa habari inahoji vitu fulani kuhusu uwajibikaji wa serikali, utayari wao kutoa maoni unatoweka."

Mhojiwa mwingine anatoa mtazamo tofauti kuhusu ukosefu wa habari zenye ukosoaji. "Serikali na sekta binafsi zimewazidi ujanja waandishi wa habari na vyombo vya habari. Huwapatia waandishi habari waitakayo na wakati fulani kuwapa pesa waandishi ili kuripoti masuala yaliyo chini yao vile watakavyo wao. Kwenye hali kama hiyo, ni ngumu kupata habari yenye ukosoaji." Mhojiwa mwingine aliongeza, waandishi wa habari "...kwa kiasi kikubwa wanahudumia matakwa ya tabaka tawala iwe ni viongozi wa serikali, wanasiasa au wafanya biashara."

Ingawa ukosefu wa uripoti wenye ukosoaji unaoisimamia serikali na wahusika wengine umeonekana kuwa tatizo katika vyombo vya habari nchini, kunaweza kuwa na ufafanuzi mwingine. Utafiti wa hivi karibuni kuhusu wasifu wa waandishi wa habari[25] ulibainisha kwamba waandishi wa habari nchini Tanzania unayatambua mambo matatu yafuatayo kama ndio majukumu yao muhimu zaidi, kuelimisha (34.3%), kuhabarisha (33.8%) na kuburudisha (20.3%). Kuhimiza uwajibikaji na kutengeneza agenda vilipata alama za chini (3.8% na 1.2%, mtawalia). Ikiwa waandishi wa habari wenyewe kwa kiasi kikubwa wanayatambua mambo hayo matatu kama majukumu yao makuu (asilimia 88.4 kwa pamoja), kunaibua maswali mazito kuhusu dhima ya vyombo vya habari nchini. Hali inatia shaka zaidi kwenye vituo vya redio ambako vipindi vyake vimesheheni habari-burudani (infotainment).

Akifafanua kuhusu changamoto nyingine inayovikabili vyombo vya habari na hivyo kuathiri ubora wa uripoti, Mhariri Mtendaji Mwandamizi alisema "...kuna masuala kadhaa ndani ya vyumba vyetu vya habari ambayo kama yatashughulikiwa, nina uhakika ubora wa uripoti utaimarika. Vyumba vingi vya habari, kama siyo vyote, vinahangaika kujiendesha na haviwezi kumudu kubaki na waandishi wengi wazuri. Waandishi [wengi] wa habari wanalipwa mishahara midogo huku wengi wao wakifanya kazi kama waandishi wa kujitegemea na kulipwa posho kidogo.'

Hoja ya kiuchumi iliripotiwa pia kwenye ripoti zilizotangulia kama moja ya changamoto kubwa

25 Katunzi, A., Ssenabulya, B. (2022). A portrait of Tanzanian journalists: A survey report, Kampala: African Centre for Media Excellence and National Endowment for Democracy

huku ikitajwa na karibu kila mhojiwa kuwa ni kichocheo kikubwa cha uripoti mbovu. Vyombo vya habari ambavyo haviwezi kujiendesha katika hali endelevu hujiweka kwenye hatari ya kutoa kazi za viwango vya chini kama siyo zisizo na maana. Changamoto za kiuchumi zina madhara makubwa. Kwa mfano, vyombo mbalimbali vya habari vimepunguza wafanyakazi wao kwani vimeshindwa kuendelea kuwa nao, leo vyumba vya habari vimebaki na wafanyakazi wachache mno. Watumishi hao wachache huwajibika kutekeleza majukumu yale yale kwa ukamilifu, jambo hili huwaongezea shinikizo. Waandishi wengi wa habari (63.1%) hapa nchini wanalipwa viwango vya chini, huku wengi wao wakilipwa chini ya shilingi za kitanzania 500,000/= kwa mwezi.[26] Kwa mujibu wa mhojiwa mmoja, jambo hili huchangia utendaji mbovu wa vyombo vya habari kwani waandishi wa habari wanashindwa kujikimu na hivyo kujikuta wanatumbukia kwenye masuala ya bahasha ya kaki.

Uwezo wa vyombo vya habari kujiendesha kibiashara ni muhimu sana katika tasnia ya habari. Athari za kutokuwa na uwezo kwa vyombo vya habari kufanya kazi zao zinaenda mbali zaidi na kuathiri jamii kwa ujumla kwani umma hukosa habari za kuaminika na zinazokidhi viwango vya ubora. Kudhoofika kwa vyombo vya habari kutokana na hali ngumu ya kifedha kunavifanya vyombo hivyo viwe katika mazingira magumu ya 'kutekwa' na wanasiasa na watu wenye nguvu katika jamii, ambao huishia kuamua hata aina ya uandishi wa habari na uripoti kwa ujumla.

Kama ilivyokuwa kwenye ripoti ya mwaka 2019, wahojiwa wengi waliibua hoja ya kutofuatwa miongozo na kanuni za kitaaluma kama sababu inayochangia uripoti mbovu. Matumizi ya habari zenye chanzo kimoja, ukosefu wa maoni kinzani, utegemezi uliopitiliza wa habari zitokanazo na matukio, matumizi yaliyopitiliza ya mtazamo mmoja na kutotoa nafasi ya haki ya kujibu kwa aliyetuhumiwa, kimsingi zilitazamwa na wahojiwa kama masuala yasiyozingatia misingi ya kitaaluma. Mengi ya masuala haya yamejumuishwa katika sera za uhariri za vyombo vya habari. Hata hivyo, wahariri na waandishi wa habari wamechagua kutozingatia matakwa haya ya kiuhariri.

Ukosefu wa mafunzo ndani ya vyumba vya habari pia kulitajwa kuwa ni miongoni mwa mambo yanayochangia hali iliyopo ya uripoti wa kiuandishi wa habari. Mhariri mmoja mwandamizi alibainisha kuwa "ni vyombo vichache tu vya habari ambavyo vinaendesha mafunzo ya ndani ya taasisi au programu wezeshi. Kwa hiyo waandishi wa habari wanapokuwa kazini hawapewi mafunzo wala kuandaliwa programu wezeshi ili kuzifanya kazi zao kwa ubora na jambo hili huathiri ubora wa kazi zao." Wakati umefika kwa vyombo vya habari kuyapa kipaumbele mafunzo kazini. Hili linaweza kufanyika kwa kuteua mwandishi mwandamizi kutoka ndani ya chumba cha habari kufanya kazi hiyo–ikiwa kuajili mtu mahsusi itaonekana kuwa ngumu. Ripoti ya Hali ya Vyumba vya Habari Tanzania ya mwaka 2022[27] ilibaini kwamba vyumba vingi vya habari (72%) havina mhariri wa kusimamia ubora na viwango.

Kwa mwaka 2022, kwa ujumla, utendaji wa redio za kimkoa umeshuka ikilinganishwa na mwaka 2018 na 2019. Tulitaka kufahamu kupitia wahojiwa ni nini kilipelekea hali hii. "Hali hiyo inaweza kuhusishwa na kupungua kwa mapato yatokanayo na matangazo ambayo nayo yanahusishwa na athari za UVIKO-19 pamoja na misaada kutoka UNESCO kufika mwisho. Redio yetu ilikuwa ikipata msaada kutoka UNESCO, na mradi ulipofika mwisho ilituathiri sana kwani tulishindwa kuziba mapengo yaliyoachwa na hali hiyo na hivyo kuathiri uzalishaji wetu wa habari", alisema mhojiwa mmoja.

Kuhusiana na uripoti wa chini wa uchumi wa buluu, kwa kauli moja, waliohojiwa walisema kwamba waandishi wa habari wanakosa ufahamu kuhusu sekta hiyo na hicho ndicho kinachopaswa kulaumiwa kwa uripoti wa chini wa suala hilo. "Ninakubaliana kabisa kuwa uripoti wa sekta hiyo ni wa chini, na ningeweza kusema kuwa suala hili limesababishwa na waandishi kukosa uelewa kuhusu sekta hii. Uchumi wa buluu ni sekta mpya na imekaa kiufundi, kwa hiyo inawataka waandishi wa habari kuielewa sekta hiyo kwa undani kabla hawajaanza kuripoti kuhusu sekta hiyo." Mhariri mwingine mwandamizi aliitaka Serikali ya Zanzibar isiwaache nyuma waandishi kwani hali hiyo itatengeneza pengo la taarifa kwa waandishi na hivyo kupelekea kuathiri ufahamu wa umma kuhusu sekta hiyo.

> "ni vyombo vichache tu vya habari ambavyo vinaendesha mafunzo ya ndani ya taasisi au programu wezeshi. Kwa hiyo waandishi wa habari wanapokuwa kazini hawapewi mafunzo wala kuandaliwa programu wezeshi ili kuzifanya kazi zao kwa ubora na jambo hili huathiri ubora wa kazi zao."

26 Katunzi, A., Ssenabulya, B. (2022). A portrait of Tanzanian journalists: A survey report, Kampala: African Centre for Media Excellence and National Endowment for Democracy

27 Katunzi, A., Ssenabulya, B. (2022). State of the newsroom in Tanzania: A survey report, Kampala: African Centre for Media Excellence and National Endowment for Democracy

5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulichunguza ubora wa uripoti nchini Tanzania, sababu za hali ilivyo sasa na changamoto zake kuu.

Mambo makuu yaliyoibuliwa

Kwa ujumla, matokeo ya mwaka 2022 yanaonesha sura mbili:

- Kwa upande mmoja, ubora wa uripoti kwa mwaka 2022 umeongezeka, ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2019, haya ni maendeleo chanya. Ubora kwenye kutumia vyanzo vingi vya habari, kuripoti kwa kutumia mtazamo zaidi ya mmoja, na kufafanua vyanzo sababishi vya habari kumeimarika. Hali hii imejitokeza zaidi kwenye TV na kidogo kwenye vituo vya redio. Kwa upande mwingine ubora wa kazi za magazeti ulikuwa wa chini, na kwenye baadhi ya vigezo vya ubora ilifikia hata kupata alama hasi. Wakati uripoti wa magazeti ukionekana kudumaa, baadhi ya vituo vya TV na redio viliboresha kazi wao.

- Kwa upande mwingine, baadhi ya vipengele vya ubora havijabadilika au vimebaki katika hali ya chini mno. Kwa mfano, palikuwa na kazi chache mno za kihabari ziliyoonyesha maoni kinzani ndani ya kazi husika (chini ya asilimia 2), na kuna kazi chache mno (chini ya asilimia 4) zilizokuwa na maoni kosoaji kwa serikali. Pia kazi za kihabari zilizojumuisha maoni kamilifu zilikuwa chache. Zaidi ya hapo, jitihada binafsi za vyombo vya habari kujitafutia habari zake zenyewe imeshuka. Vile vile nafasi itolewayo kwa haki ya kujibu ikiwa mtu atatuhumiwa kufanya makosa bado haitoshi licha ya kuwa imeimarika kidogo. Kwa mujibu wa misingi ya kimaadili, inapaswa kuwa asilimia 100, lakini kwa sasa iko chini ya asilimia 50.

Kuna mabadiliko makubwa miongoni mwa vyombo vya habari, vile vilivyokuwa miongoni mwa vilivyoongoza mwaka 2019, kwa mwaka 2022 vimejikuta mwishoni mwa msimamo. Ubora wa kazi za baadhi ya vituo vya redio za kimkoa umekuwa tofauti na wa miaka iliyopita, wakati kwa vyombo vingine vya habari vikiwamo vile vinavyomilikiwa na serikali vimefanya vizuri kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na mwaka 2019.

Uripoti wa mitazamo mingi zaidi, usuli wa kihistoria na vyanzo sababishi ni maeneo ambayo hali ya uripoti wake iliboreshwa. Utofauti huu wa kiutendaji kwenye ubora una uhusiano na sababu kuu za ukosefu wa rasilimali za kiuchumi za kusimamia shughuli za kiuandishi wa habari ili kufikia uripoti bora.

Changamoto kuu

- Mazingira ya kifedha imekuwa hoja kuu kwa vyombo vyingi za habari ambapo baadhi yake haviwezi kumudu kubaki na waandishi wengi wazuri. Vyombo vingi vya habari vimepunguza wafanyakazi wao kwa sababu ya changamoto za kiuchumi, na watumishi waliobaki wanatarajiwa kutekeleza idadi ile ile ya majukumu kwa ukamilifu. Changamoto hii inachangia kwa kiasi kikubwa kudumaa kwa uripoti wa vyombo vya habari nchini.

- Wasiwasi kuhusu uhuru wa kujieleza kwenye uripoti kuna nafasi yake kubwa. Ingawa baadhi ya vyombo vya habari vinahisi unafuu mkubwa kwenye mazingira ya kisiasa, vingine bado havina uhakika. Hali hii ya kutokuwa na uhakika inachangia ukosefu wa habari zenye mwelekeo wa kusimamia wajibikaji kwa serikali na wahusika wengine.

- Kutofuata miongozo ya kiuhariri ni sababu nyingine ya uripoti wa chini kwenye baadhi ya maeneo ya viashiria vya ubora, kama vile ukosefu wa vyanzo vya habari, ukosefu wa kutoa haki ya kujibu tuhuma na matumizi yaliyopitiliza ya uripoti usiokuwa na usawa. Vigezo hivi vimewekwa vizuri kwenye miongozo ya kimaadili kwa sekta nzima ya habari nchini na kwenye miongozo ya kihariri kwenye vyombo vya habari.

MAPENDEKEZO

Kulingana na matokeo haya, utafiti huu unapendekeza hatua kadhaa kwa wahusika tofauti.

Mapendekezo kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari

Vyombo vya habari vinapaswa kuendeleza jitihada zake za kuimarisha ubora wa uripoti kwenye uandishi wa habari licha ya mazingira magumu ya kiuchumi. Baadhi ya maeneo tayari yameimarika, lakini bado maeneo mengine yamebaki chini mno. Kwa mfano, kuweka usawa kwenye habari kwa misingi ya kutoa maoni

kinzani ni jambo ambalo bado linahitaji maboresho kama ilivyo kwa utoaji wa habari zenye kuangazia uwajibikaji.

Vyombo vya habari vinashauriwa kutumia matokeo ya utafiti huu kuimarisha uripoti nchini. Vilevile vinashauriwa kurejea kwenye kipimo cha ubora ambacho kinaonesha ubora wa kila chombo (individual performance sheet) ili kufanyia kazi maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa. Pia, vinashauriwa kutumia matokeo ya utafiti huu na kipimo cha ubora kuandaa mafunzo ya ndani kuhusiana na changamoto za uripoti. Ili mafunzo hayo yawe fanisi, inapendekezwa kila chombo cha habari kiteue mwandishi mwandamizi kutoka ndani ya chombo husika kusimamia mafunzo hayo, kama kuajiri mtu huyo itashindikana.

Vyombo vya habari vinapaswa kusimamia taratibu zao za ndani kuhakikisha viwango vya maadili na uhariri vinazingatiwa kikamilifu. Kutokana na changamoto kubwa za kiuchumi, ni muda mwafaka sasa kwa vyombo vya habari kuangalia njia mbadala za kibiashara za kujiongezea mapato.
Mapendekezo kwa taasisi zinazosaidia vyombo vya habari

Taasisi mbalimbali nchini zinafanya kazi ya kuimarisha ubora wa uripoti kwa vyombo vya habari. Taasisi hizi zinashauriwa kuandaa programu za mafunzo ya uripoti bora wa vyombo vya habari kwa namna ambayo itaondoa changamoto zilizobainishwa kwenye ripoti hii.

Mapendekezo kwa washirika wa maendeleo

Washirika wa maendeleo pia wanaalikwa kusoma matokeo ya utafiti huu ili jitihada zao na hatua wanazozichukua ziweze kuboresha mazingira ya vyombo vya habari nchini. Ripoti hii inaweza pia kutumika kama chanzo cha ushauri kwa washirika wa maendeleo maalum, kwani utafiti huu umebainisha vyombo vya habari vinavyofanya vizuri na vinavyoweza kuigwa.

Mapendekezo kwa Serikali

Wakati Serikali ikifanya mapitio ya Sheria ya Huduma za Habari ya 2016, mapitio hayo yalenge kutengeneza mazingira rafiki kwa waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao bila upendeleo na vikwazo.

Mapendekezo kwa taasisi za mafunzo ya uandishi wa habari

Kwa taasisi zinazoandaa waandishi wa habari wa siku za usoni wa ngazi mbalimbali (vyuo na vyuo vikuu), inapendekezwa kwamba wajumuishe vigezo vya ubora vinavyotumika kwenye utafiti huu kwenye mitaala yao. Hii itawasaidia wanafunzi wa uandishi wa habari kuvielewa vizuri vigezo hivyo tangu hatua za awali wakiwa vyuoni na hivyo kuvitumia vigezo hivyo mapema wakati wakiingia kwenye utekelezaji wa majukumu ya taaluma yao.

Viambatisho

Kiambatisho I

Mbinu za Utafiti (Methodolojia)

Ili kupima ubora wa uripoti wa vyombo vya habari, utafiti huu unatumia uchambuzi wa matini (content analysis), mbinu inayofuata utaratibu maalum wa kuchambua kazi zinazozalishwa na vyombo vya habari (habari, makala, vipindi, n.k.) kwa kuzingatia vigezo mahsusi, pamoja na kufanya mahojiano na wadau wa habari.

Quality criteria Vigezo vya ubora

Utafiti huu unatumia neno "ubora" kama muhtasari wa dhana inayobeba vigezo mbalimbali vya ubora, hii ni kwa sababu siyo rahisi kuupima ubora. Badala yake, inawezekana kupima vigezo mbalimbali halisi vya ubora, ambavyo ni vipengele tofauti vya ubora wa jumla. Vigezo vya ubora vilivyotumika kwenye utafiti huu vinatokana na nadharia ya uandishi wa habari na uhalisia wa kazi ya uandishi wa habari. Vigezo hivi viliandaliwa kwenye warsha iliyowakutanisha wadau mbalimbali wa habari wakiwemo wahariri, waandishi wa habari, taasisi zinazosaidia vyombo vya habari na wawakilishi kutoka serikalini. Vigezo hivi vimekuwa vikipitiwa kila mwaka na wadau hao. Vigezo vya ubora vinaangazia vipengele vingi vya uandishi wa habari kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini:

Vigezo vya ubora	Kigezo cha ubora – ni kipi cha kuangalia
Weledi	■ Uripoti unaozingatia vyanzo vingi vya habari ■ Kuripoti zaidi ya habari za matukio, na kufanya jitihada binafsi kupata habari zisizo za matukio
Utoaji wa taarifa kamili	■ Uripoti wenye mitazamo mbalimbali ■ Uripoti wa vyanzo sababishi vya tukio/ suala/tatizo ■ Uripoti unaozingatia usuli wa kihistoria wa tukio/suala/tatizo ■ Kutoa maoni ya aina mbalimbali kuhusu tukio/ suala/tatizo ■ Kutoa maoni kinzani na hivyo kuwa na usawa.
Kueleweka na hadhira	■ Msingi mzuri wa habari husika (Haikujumuishwa kwenye utafiti huu) ■ Muundo mzuri wa kazi ya kihabari (mtiririko, muunganiko kimantiki) ■ Matumizi ya takwimu katika muktadha mzuri (Haikujumuishwa kwenye utafiti huu)
Maadili	Kuzingatiwa kwa haki ya kujibu tuhuma (ikiwa kuna tuhuma dhidi ya mtu au taasisi)

Upatikanaji wa sampuli za vyombo vya habari

Vyombo vya habari (29) vilichaguliwa kwa mwaka 2022, vikijumuisha magazeti (9), vituo 15 vya redio, na vituo vitano (5) vya televisheni. Uchaguzi huu unawakilisha aina mbalimbali za vyombo vya habari, vile vinavyomilikiwa na serikali, watu/taasisi binafsi, vyombo vya habari vya kitaifa na vya kimkoa.

Uchaguzi wa kazi za kihabari

Utafiti huu ulitumia mbinu ya "wiki bandia" (artificial week sampling) kama njia ya kupata sampuli ili kuhakikisha kwamba sampuli inayopatikana inawakilisha vizuri kazi za kihabari halisi zilizokusanywa. Siku kumi (10) ndani ya wiki halisi kumi zilichaguliwa, na kazi zilizofanyiwa uchunguzi kwa vyombo vyote vya habari zilichukuliwa kutoka kwenye siku hizi kumi. Kipindi cha wiki hizo kumi kilikuwa ni kutoka mwezi Machi mpaka Juni, 2022. Baadhi ya kazi kutoka kwenye baadhi ya vyombo vya habari zilichukuliwa nje ya kipindi hiki kwani idadi ya sampuli iliyokuwa ikihitajika haikuwa imepatikana ndani ya muda halisi uliokuwa umetengwa awali kwa ajili ya kupata sampuli.

Uchaguzi wa kazi za kufanyiwa uchunguzi

Kwa upande wa magazeti, kazi (8) kwa siku zilichaguliwa. Kazi hizi zilijumuisha habari za ukurasa wa mbele wa magazeti, habari zinazoongoza kwenye kila ukurasa, makala, maoni, uchambuzi, na tahariri. Habari za michezo, burudani na za kimataifa hazikuchaguliwa. Kwa upande wa televisheni na redio, habari nne za mwanzo kwenye taarifa kuu ya habari ya siku zilichaguliwa pamoja na vipindi vitatu vya siku hiyo. Kwenye mazingira ambayo vipindi vyote vitatu ilikuwa vigumu kupatikana kwenye siku husika, basi vipindi hivyo vilivyokosekana vilichukuliwa kutoka siku inayofuata ndani ya wiki hiyo. Kwa vipindi vyenye vipengele mbalimbali, ni kipengele kimoja tu kilichukuliwa na kujumuishwa kwenye utafiti.

Kurekodi kazi za Redio na Televisheni

Kabla ya kurekodi kazi kutoka kwenye redio na televisheni husika, watatafiti walipitia ratiba za vipindi vya redio na televisheni hizo ili kuchagua vipindi vitakavyorekodiwa. Kwa redio za mikoani, kazi ya kurekodi vipindi ilifanywa na wasaidizi kutoka kwenye redio husika, huku kazi ya kurekodi vipindi vya redio na TV zilizobaki ilifanywa na watafiti wasaidizi kutoka SJMC.

Uhakikisho wa ubora wa kazi zilizorekodiwa na usimbaji

Uhakikisho wa ubora ulijumuisha mchakato makini wa kuhakikisha kwamba kazi zote zilizorekodiwa zilikuwa kamili na kusimbwa vizuri. Kazi zote za kwenye magazeti na fasili za redio na TV zilihifadhiwa ili ziweze kurejelewa pindi pakitokea mahitaji ya kufafanua kitu chochote kuhusiana na usimbaji.

Uchunguzi na uchambuzi wa data

Data kutoka kwenye usimbaji zilichunguzwa zaidi ili kuona kama kuna usahihi na mwendelezo na kisha kuwekwa pamoja kwenye faili la SPSS. Uchambuzi ulifanyika kwa kutumia nyenzo za uchambuzi zilizozoeleka – kuhesabu idadi ya ujitokezaji na mlinganisho – wa kazi halisi na iliyosimbwa upya kwenye vigezo vya ubora.

Kiambatisho 2

Ukokotoaji wa Kipimo cha Ubora

Kipimo cha ubora kwa mwaka 2022 kiliboreshwa kidogo na kukokotolewa kwa vigezo 9 vya ubora:

- Visababishi vya uripoti: % ya kazi zilizozalishwa kwa jitihada binafsi za chombo cha habari (=si habari za matukio).
- Vyanzo vingi vya habari: % ya kazi zilizotumia vyanzo viwili au zaidi vya habari.
- Idadi ya mitazamo: % ya kazi zilizotumia angalau mitazamo miwili.
- Idadi ya maoni: % ya kazi zilizotumia angalau maoni 2.
- Maoni kosoaji kwa serikali: % ya kazi zilizokuwa na maoni kosoaji kwa serikali.
- Kuripoti vyanzo sababishi vingi: % ya kazi zilizotumia angalau na aya 2 (kwenye magazeti) au sentensi 2 (kwenye redio na TV) zikitoa taarifa kuhusu vyanzo sababishi au sababu ya suala linalojitokeza kwenye habari kuu.
- Kuripoti kwa mapana usuli wa kihistoria: % ya kazi ambazo zilitumia angalau aya 2 (kwa magazeti) au sentensi 2 (kwa redio na TV) zikitoa usuli wa kihistoria kuhusu habari husika.
- Muundo: % ya kazi zilizokuwa na muundo mzuri sana ulioziunganisha vizuri aya na vipengele vingine tofauti vya matini.
- Haki ya kujibu tuhuma: % ya kazi zilizotoa nafasi ya haki ya kujibu tuhuma pindi mtu au taasisi inapotuhumiwa kwa mambo mabaya.

Pale ilipojitokeza idadi ya kazi zilizotuhumu watu/taasisi kuwa chini ya 5, kigezo cha "haki ya kujibu tuhuma" hakikutumika. Kwa hiyo, kipimo cha ubora kilijielekeza zaidi kwenye vigezo nane kwa vyombo vya habari ambavyo havikuwa na kazi za kutosha zilizohitajika kwenye kigezo hiki, na viashiria tisa kwa vyombo vya habari vilivyokuwa na kazi za kutosha kwenye kigezo hiki.

Kiambatisho 3

Mkoa	Idadi ya habari	Asilimia ya habari zote	Mkoa	Idadi ya habari	Asilimia ya habari zote
Dar es Salaam	180	19.4%	Lindi	17	1.8%
Dodoma	106	11.4%	Morogoro	17	1.8%
Arusha	72	7.7%	Ruvuma	17	1.8%
Tabora	54	5.8%	Shinyanga	17	1.8%
Mbeya	52	5.6%	Mara	16	1.7%
Kaskazini Pemba	47	5.1%	Kagera	15	1.6%
Mwanza	45	4.8%	Njombe	15	1.6%
Mjini Magharibi	32	3.4%	Iringa	13	1.4%
Kaskazini Unguja	22	2.4%	Manyara	12	1.3%
Kilimanjaro	21	2.3%	Songwe	10	1.1%
Mtwara	21	2.3%	Simiyu	9	1.0%
Kusini Pemba	21	2.3%	Singida	7	0.8%
Geita	20	2.2%	Kigoma	6	0.6%
Pwani	20	2.2%	Rukwa	5	0.5
Kusini Unguja	20	2.2%	Katavi	2	0.2%
Tanga	19	2.0%	Lindi	17	1.8%

Habari zifuatazo zimeondolewa kwenye jedwali hili: habari zilizokuwa na mlengo wa kimada zaidi na sio kijiografia (866), zilizoangazia mkoa zaidi ya mmoja (67) na zilizoangazia nje ya nchi (24).

UBORA WA MAUDHUI YA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA TANGU 2017

Supported by

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Embassy of Switzerland in Tanzania
Ubalozi wa Uswisi Tanzania

Kingdom of the Netherlands

Imetolewa na
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma
S.L.P 4067 Mikocheni B Makaburi Street, Plot Block D, No.34
Tel: +255 22 2700756 Dar es Salaam, Tanzania
Email: sjmc@udsm.ac.tz | yearbookmediatz@gmail.com